# JARIDA LA MKOA WA RUVUMA

## SEKTA YA ELIMU KATIKA MKOA WA RUVUMA



Serikali Inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan imetoa shilingi bilioni 7.7 kujenga sekondari mpya 11 za mfano na zenye mazingira ya kuvutia kwa walimu na wanafunzi katika Mkoa wa Ruvuma

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA**

**KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI OFISI YA MKUU WA MKOA WA RUVUMA**

Haki zote zimehifadhiwa.Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupigachapa, kutoa nakala kivuli au kutoa baadhi ya maandishi ya Jarida hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya mwandishi kwa maandishi.

Jarida limehaririwa na Albano Midelo wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini (GCU) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

Limesanifiwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

**YALIYOMO**

***Shukrani***

***Utangulizi***

***SURA YA KWANZA***

***SEKTA YA ELIMU KWA UJUMLA MKOANI RUVUMA***

*1. Elimu ya Awali na Msingi kwa ujumla mkoani Ruvuma*

*2.Elimu ya sekondari mkoani Ruvuma*

*3.Utekelezaji Program ya elimu bila malipo*

*4.Wanafunzi Mpitimbi wamshukuru Rais kwa mabweni*

## *SURA YA PILI*

## *UJENZI WA MADARASA YA UVIKO KATIKA RUVUMA*

*I. Sh.bilioni 10 za UVIKO zilivyojenga madarasa 500 mkoani Ruvuma*

*II.Wanafunzi Ruvuma wamshukuru Rais kwa ujenzi wa madarasa*

## *SURA YA TATU*

## *UBORESHAJI ELIMU YA SEKONDARI TANZANIA*

*A.Ujenzi wa sekondari kupitia program ya SEQUIP Ruvuma*
*B.Sekondari mpya ya Halmashauri ya Mbinga*

*C.Mradi wa sekondari mpya ya wasichana ya Mkoa wa Ruvuma*

*D.Bilioni 20 zilivyojenga shule mpya 11 na madarasa 656 Ruvuma*

*E. Mradi wa shule mpya ya sekondari ya Luhira Songea*

*F.Mazingira rafiki ya kusomea sekondari ya Mbinga*

*G.Songea wanavyojivunia sekondari mpya ya Kizuka*

*H.Mradi wa ujenzi sekondari moya ya Madaba*

*I.Mradi wa sekondari mpya tatu za mfano Tunduru*

*J.Tunduru wanavyojivunia mradi wa sekondari moya*

*K.Mradi wa ujenzi wa sekondari mpya ya Msisima Namtumbo*

*L.Ujenzi wa sekondari mpya Kata ya Majimaji Tunduru*

*M.Serikali yatoa bilioni 1.4 kujenga sekondari mpya Tunduru*

*N.Sekondari ya mfano Kata ya Kizuka Songea*

## *SURA YA NNE*

## *UJENZI WA MADARASA MAPYA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI RUVUMA*

*I.Serikali yatoa bilini 3.2 kujenga madarasa mapya Ruvuma*

*II.Bi;ioni 3.2 zilivyojenga madarasa mapya 156 Ruvuma*

*III.Mbinga Girls wamshukuru Rais kwa ujenzi wa madarasa*

*IV.Makita Sekondari watuma salamu za shukurani kwa Rais*

*V.Songea wakabidhi vyumba vya madarasa 76*

*VI.Halmashauri tatu za Songea zakabidhi madarasa 96*

## *SURA YA TANO*

## *UTEKELEZAJI WA MRADI WA BOOST*

*A.Mradi wa BOOST kujenga madarasa 12,000 katika shule za msingi*

*B.Mkoa wa Ruvuma unavyotekeleza mradi wa BOOT*

*C.Ujenzi wa madarasa mapya katika shule za msingi*

## *SURA YA SITA*

## *UKARABATI WA SEKONDARI KONGWE MKOANI RUVUMA*

*1. Ukarabati wa sekondari kongwe ya wavulana Songea*

*2.Sekondari kongwe ya Tunduru ilivyokarabatiwa*

*3.Ukarabati wa sekondari ya Songea Girls*

*4.Ukarabati wa sekondari ya Kigonsera Mbinga*

## *SURA YA SABA*

## *UJENZI WA VYUO VYA VETA MKOANI RUVUMA*

*A.Ujenzi wa chuo cha ufundi stadi VETA cha Nyasa*

*B.Kifahamu chuo cha ufundi stadi cha Songea*

*C.Mradi wa chuo cha ufundi stadi Namtumbo*

## *SURA YA NANE*

## *ELIMU NYINGINE ZINAZOTOLEWA MKOANI RUVUMA*

*1.Elimu maalum,elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi*

*2. Watoto wenye ulemavu 149 wagundulika Madaba*

*3.Songea yajenga shule mpya ya elimu maalum*

*4.RC Ruvuma azindua miongozo mitatu ya elimu*

## *SURA YA TISA*

## *HABARI PICHA KATIKA SEKTA YA ELIMU RUVUMA*

*A.Ukaguzi mradi wa sekondari ya Limbu Nyasa*

*B.RAS Ruvuma akerwa na matokeo mabaya sekondari ya Makita*

*C.Menejimenti Ruvuma yapongeza ujenzi sekondari ya Lusonga*

*D.Sekondari ya mfano wilayani Mbinga*

*E.Mradi wa sekondari mpya ya Mababa*

*F.RC Ruvuma akagua mradi wa ujenzi sekondari ya Mkoa*

*G.Mkuu wa mkoa akagua samani za sekondari ya wasichana ya mkoa*

*H.Ifahamu sekondari ya mfano mkoa wa Ruvuma*

*I.Utekelezaji wa program ya SEUIP mkoani Ruvuma*

*J.Ziara ya RC Ruvuma kukagua miradi ya maendeleo*

*K.Sekondari ya mfano katika Manispaa ya Songea*

*L.Milioni 470 zilivyojenga sekondari mpya Songea*


## *SHUKRANI*

Kwa namna ya pekee namshukuru mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia afya njema hivyo kufanikisha kuandika Jarida la Mkoa wa Ruvuma katika sekta ya ***elimu ambalo linaangazia miradi mbalimbali ya elimu inayotekelezwa mkoani Ruvuma na sekta ya elimu kwa ujumla zikiwemo VETA,Elimu maalum,Elimu nje ya mfumo rasmi na elimu ya watu wazima.***

# UTANGULIZI

Sekta ya Elimu Mkoani inafanya kazi kwa ushirikiano na Halmashauri, Idara ya uthibiti ubora wa elimu, Idara ya Tume ya utumishi wa walimu (TSC), Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, vyuo vya Ualimu na Mamlaka ya vyuo vya ufundi (VETA), Chuo kikuu Huria cha Tanzania (OUT) na maktaba ya Mkoa. Jedwali lifuatalo linaainisha mchanganuo wa Taasisi za elimu zilizopo Mkoa wa Ruvuma.

**Jedwali linaonesha Idadi ya taasisi za elimu katika Halmashauri za Mkoa wa Ruvuma hadi kufikia Novemba, 2022**

| Halmashauri | Elimu ya Awali | | Elimu ya Msingi | | Elimu ya Sekondari | | Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi | | VETA | | Vyuo vya Ualimu | | Vyuo vya Elimu ya Juu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | *S | *B | S | B | S | B | S | B | S | B | S | B | S | B |
| Madaba | 28 | 1 | 28 | 1 | 10 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mbinga dc | 164 | 3 | 164 | 3 | 31 | 16 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mbinga TC | 72 | 9 | 72 | 9 | 15 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Namtumbo | 108 | 5 | 108 | 5 | 26 | 8 | 1 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Nyasa | 111 | 0 | 111 | 0 | 16 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Songea DC | 78 | 3 | 78 | 3 | 17 | 5 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Songea MC | 82 | 14 | 82 | 14 | 25 | 18 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 1 |
| Tunduru | 151 | 1 | 151 | 1 | 24 | 2 | 1 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **794** | **36** | **794** | **36** | **164** | **59** | **5** | **4** | **3** | **1** | **1** | **2** | **1** | **1** |
| **Jumla Kuu** | **830** | | **830** | | **223** | | **9** | | **4** | | **3** | | **2** | |

# *SURA YA KWANZA*

## *SEKTA YA ELIMU KWA UJUMLA MKOANI RUVUMA*

### *1.ELIMU YA AWALI NA MSINGI*



***Pichani ni wadau wa elimu mkoani Ruvuma katika picha ya Pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas***

Elimu ya Awali ni hatua muhimu ya Maandalizi katika mzunguko wa elimu. Serikali ya Tanzania imeirasmisha na kujumuisha elimu hii kwenye mfumo rasmi wa elimu na kuagiza kila shule ya msingi iwe na darasa la elimu ya awali litakaloandikisha watoto wenye umri wa miaka 5-6. Elimu ya Awali inachukua miaka miwili bila ya mitihani ya kuwapandisha watoto.

Kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Mafunzo (ETP) ya mwaka 1995, Elimu ya Awali inakusudiwa kuhimiza maendeleo ya jumla ya haiba ya mwanafunzi, sifa za kimwili, kiakili na kimaadili na uwezo.

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya shule za msingi **828**, kati ya hizo za Serikali ni **793** na zisizo za Serikali ni **35**. Mkoa umeanza zoezi la uandikishaji wa wanafunzi wa awali kwa mwaka wa masomo utakaoanza mwezi januari 2023

Mkoa wa Ruvuma hadi kufikiaNovemba, 2022 una idadi ya wanafunzi wa darasa la Awali hadi la VII **353,509** Kati yao wavulana **175,368** na wasichana**178,141.**

**ii) Walimu wa Shule za Msingi hadi Novemba, 2022**

Hadi kufikia Novemba, 2022 mahitaji ya walimu wa shule za msingi ni **10,071**, Waliopo **6,214** hivyo upungufu ni walimu **3,857**

**iii) Hali ya ufaulu wa mtihani wa darasa la saba 2021**

Mwaka **2021** wanafunzi wa darasa la saba wapatao **39,614 walisajiliwa** kufanya mtihani wa darasa la saba. Wanafunzi waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi walikuwa ni **39,604** sawa na asilimia **99.9.** Wanafunzi waliofaulu mtihani walikuwa **28,356** sawa na asilimia **73.1** ambapo wanafunzi wote waliofaulu wamechaguliwa kujiunga na elimu ya sekondari.

Hadi kufikia Novemba, 2022 Mkoa una mahitaji ya madawati **126,248** yaliyopo ni **102,430** na upungufu ni **23,818** Aidha, Mkoa kwa kushirikiana na Wilaya zake umeendelea na jitihada mbalimbali ili kuweza kuondoa upungufu uliopo

Hadi kufikia Novemba, 2022 Mkoa una mahitaji ya vyumba vya madarasa **10,003**; yaliyopo ni **6,294** na upungufu ni **3,709.** Kwa upande wa matundu ya vyoo Mkoa ulikuwa na mahitaji **17,372** yaliyopo ni **9,977** na upungufu ni **7,395**.



***Pichani ni Neema Maghembe Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea akizungumzia serikali ilivyoa shilingi milioni 55 kujenga madarasa ya awali.***

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Neema Maghembe amesema fedha hizo zimetolewa na Ofisi ya Rais- TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikiwa ni fedha za utekelezaji wa mradi wa kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa Elimu ya Msingi kwa awamu ya pili (GPE-LANES II).

Amesema utekelezaji wa mradi huo utahusisha ujenzi wa madarasa mawili (02), ujenzi wa matundu manne (04) ya vyoo vya kawaida na matundu mawili (02) ya vyoo vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu, ununuzi au

utengenezaji wa samani za ndani viti na meza, ununuzi wa matanki mawili (02), mikeka mitano (05), shubaka, bembea (michezo ya wanafunzi), maandalizi ya viwanja vya michezo, ununuzi wa kizima moto, kutengeneza mfereji wa maji pamoja na kigundua moto.

Ameongeza kuwa Mradi wa kuimarisha Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa Elimu ya Msingi Awamu ya Pili (GPE-LANES II) ni msaada, hivyo haupaswi kulipa kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

Vilevile Mkurugenzi Neema amebainisha kuwa kulingana na maelekezo ya Serikali, mradi huo utatekelezwa kwa kutumia Force Account na unatakiwa kukamilika kabla au ifikapo tarehe 15 Juni, 2023.

Uongozi wa Halmashauri unatoa shukrani kwa Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kuleta fedha kwa ajili ya kuboresha huduma za kijamii hususani Elimu.

## *II.ELIMU YA SEKONDARI MKOANI RUVUMA*



***Pichani ni moja ya majengo katika shule ya sekondari Tunduru***

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya shule za sekondari **218** zikiwemo **160** za Serikali na **58** ni shule za binafsi. Kati ya shule **160** za Serikali, shule tano **(5)** ni za bweni na shule **155** ni za kutwa. Kati ya shule **218** zenye kidato cha tano na sita ni **35** (Serikali **23** na zisizo za Serikali **12**).

**i) Walimu wa Shule za Sekondari hadi Novemba ,2022**

Hadi kufikia No vemba ,2022 mahitaji ya walimu wa shule za sekondari ni **4,041**, Waliopo **3,523** hivyo upungufu ni walimu **518**

**ii) Walimu wa Ajira Mpya**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwezi **Juni, 2022** ilitoa ajira kwa walimu katika Mikoa yote ya Tanzania Bara ambapo Mkoa wa Ruvuma ulipangiwa jumla ya walimu **389 (Me 279, Ke 110)** kwa shule za Msingi na Sekondari. Aidha, walimu **213 (Me 175, Ke 38)** walipangwa katika shule za Sekondari ambapo kati yao walimu **212 (Me 174**, **Ke 38**) tayari wameripoti katika shule walizopangiwa. Kwa upande wa shule za Msingi walipangwa walimu **176** na wote wameripoti

**iii) Hali ya ufaulu wa kidato cha nne**

Mkoa wa Ruvuma kitaaluma unaendelea kufanya jitihada za makusudi ili kuweza kupata matokeo mazuri zaidi. Mwaka 2021 Mkoa ulikuwa na ufaulu wa asilimia **90.1**% Juhudi za kupandisha ufaulu na kudhibiti udanganyifu ziliendelea kufanyika

**iv) Ufaulu wa kidato cha Sita 2022**

Mkoa umeendelea kufanya jitihada kuboresha ufaulu wa wanafunzi katika matokeo ya kidato cha Sita. Mwaka 2022 Mkoa umepandisha ufaulu na kupata wastani wa ufaulu wa 99.9.

**v) Miundombinu ya shule za sekondari**

Miundombinu ya shule za sekondari imekuwa ikijengwa ili kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na kufundishia yakiwemo madarasa, majengo ya utawala, nyumba za walimu, Mabweni, Maktaba, maabara na vyoo

**vi) Samani**

Hadi kufikia Novemba, 2022 hali ya samani katika shule za sekondari kwa ajili ya wanafunzi ni, mahitaji ya meza ni **88,350,** zilizopo zikiwa ni **83,346** na Upungufu ni **5,004.** Mahitaji ya viti ni **88,506**, vilivyopo ni **82,766** upungufu ni viti **5,740**.

**vii) Maabara katika shule za sekondari Ruvuma**



***Katikati aliyeshika kiuno ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Ndugu Stephen Ndaki akikagua moja ya maabara katika sekondari mpya ya Lusonga Halmashauri ya Mji wa Mbinga***

Maabara za sayansi katika sekondari mkoani Ruvuma hadi kufikia Novemba, 2022 ni kama ifuatavyo; mahitaji ni **655,** zilizopo ni **484** pungufu ni **171**.

## ***III.UTEKELEZAJI WA PROGRAM YA ELIMU BILA MALIPO***



***Pichani ni baadhi ya wanafunzi wa Songea Girls ambapo hivi sasa serikali inatoa elimu bure kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita***

Sera ya utoaji wa Elimu Bila Malipo inaendelea kutekelezwa ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai 2022 hadi Oktoba 2022 Mkoa umepokea kiasi cha **5,090,198,358.75** ambazo zimesaidia katika uendeshaji wa shule na kuboresha na kuimarisha tendo la ufundishaji na ujifunzaji kwa shule za msingi na sekondari ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa upatikanaji wa

vitabu vya kiada na ziada. Aidha, Mkoa kwa kushirikiana na Halmashauri unaendelea kufuatilia na kutekeleza kwa ufanisi utoaji wa elimu bila malipo ili fedha ya Serikali inayowekezwa iweze kutoa Matokeo chanya katika kuongeza ufaulu wa wanafunzi katika Mitihani ikiwemo kuimarisha taaluma na elimu kwa ujumla na hivyo kujenga jamii yenye uelewa na kujiletea maendeleo

## IV.WANAFUNZI MPITIMBI SEKONDARI WAMSHUKURU RAIS KUWAJENGEA BWENI



WANAFUNZI wa shule ya Sekondari Mpitimbi Halmashauri ya wilaya Songea,wameishukuru serikali kupitia Halmashauri ya wilaya Songea kuwajengea bweni jipya na la kisasa lililo saidia kumaliza changamoto ya malazi na kupata muda wa kutosha wa kujisomea.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti walisema kuwa,jitihada za Halmashauri ya wilaya kuboresha miundombinu mbalimbali ikiwamo ujenzi wa bweni hilo na vyumba viwili vya madarasa vilivyojengwa kwa fedha za mpango

wa maendeleo kwa ustawi wa jamii na mapambano dhidi ya Covid-19 ni kielelezo cha namna serikali ya awamu ya sita inavyowajali wananchi.

Salma Abdi mwanafunzi wa kidato cha tano alisema,awali walilazimika kulala kwenye bweni dogo na chakavu ambalo halikuwa salama kwa afya zao kutokana na sakafu yake kuwa ya udongo,hivyo kusababisha kutokea magonjwa ya mara kwa mara.

Alisema, baada ya kupata bweni jipya wanafunzi wa shule hiyo wataendelea kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan aliyedhihirisha nia yake ya kumkomboa mtoto wa kike kusoma kwa bidii.

Naye mwanafunzi mwingine Jackline Panaska,amemshukuru mbunge wa Jimbo la Peramiho Jenista Mhagama na wananchi wa kata ya Mpitimbi, kwa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa bweni hilo na miundombinu mingine ya shule ambapo nguvu zao zimesaidia kupata bweni la kisasa ambalo ni mkombozi na kuhaidi kulitumia kuongeza muda wa kujisomea ili waweze kutumiza ndoto zao.

Aidha,ameiomba serikali kupitia wakala wa maji safi na salama(Ruwasa)wilaya ya Songea, kufikisha huduma ya maji hadi bwenini ili wayatumie kufanya usafi hasa kwenye vyoo ili kuwaepusha kupata magonjwa mbalimbali.

“tunaishukuru serikali yetu na mbunge wa jimbo letu mama yetu Jenista Mhagama kwa jitihada zake,hata hivyo tunaomba huduma ya maji safi na salama yafike bwenini kwa kuwa mazingira yetu yanahitaji maji mengi kutokana na wingi wa wanafunzi tuliopo”alisema.

Mwalimu wa ujenzi wa shule hiyo Mathew Haule alisema, walipokea jumla ya Sh.milioni 80 kutoka serikalini kwa ajili ya ujenzi wa bweni hilo ambapo fedha zilizotumika ni Sh. milioni 79,995.561 na kubaki shilingi 4,400.

Mwalimu Mathew alisema, hatua ya Serikali kujenga bweni kwa ajili ya wanafunzi wa kike imewasaidia wanafunzi hao kupata elimu bora na kuongezeka kwa taaluma ikilinganishwa na miaka ya nyuma.

Alisema,bweni hilo limejengwa mahususi kwa lengo la kuwasaidia wanafunzi wa kike wa kidato cha tano na sita kutoka katika makazi yao ili kufika shule kwa wakati na kuwawezesha kupata muda mwingi wa kujisomea na sehemu salama ya kuishi wakiwa shuleni.

“apo awali wanafunzi walitumia bweni dogo ambalo halikuwa salama kwa afya zao  kwa kuwa chini kulikuwa na udongo,hivyo kusababisha kupata mafua mara kwa mara,tunaishukuru sana serikali kwa kujenga bweni jipya”alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya wilaya Songea Neema Maghembe alisema, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 serikali imetumia  jumla ya Sh.milioni 480 kwa ajili ya kujenga mabweni 6 katika shule za sekondari.

Aidha Maghembe alieleza kuwa, mwaka wa fedha 2022/2023 serikali imepanga kutumia Sh.milioni 320 kujenga mabweni mengine 4 ambapo wameshapokea Sh.milioni 160 kati ya Sh.milioni 320 kwa ajili ya kujenga mabweni 2.Mkurugenzi huyo,ameishukuru serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuikumbuka Halmashauri hiyo  kwa kuipa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi na kuboresha huduma mbalimbali za kijamii.



**Moja ya mabweni ambayo ambalo limejengwa katika shule ya sekondari Mpitimbi Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma hivyo kumaliza kero ya Watoto wa kike kutoka mbali ya shule hivyo kuwa katika hatari ya kufanyiwa vitendo vya kikatili na kupata mimba za utotoni**

## SURA YA PILI

## MIRADI YA MAENDELEO SEKTA YA ELIMU

### I.SH.BILIONI 10 ZA UVIKO ZILIVYOJENGA MADARASA 500 RUVUMA




MKOA wa Ruvuma umepokea mgao wa jumla ya zaidi ya shilingi bilioni 10 ya fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na UVIKO -19 (mradi na 5441-TCRP).

Afisa Elimu Mkoa wa Ruvuma Hakimu Mafuru akitoa taarifa hiyo amesema mgao huo wa fedha kwaajili ya vyumba 448 vyenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 8 kwaajili ya Shule za Sekondari,vyumba 52 katika vituo shikizi za shule ya Msingi zaidi ya shilingi bilioni moja na mabweni matatu yenye thamani ya shilingi milioni 240.

Amesema kupitia mpango huo wa Maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO 19 jumla ya wanafunzi 28,356 sawa na asilimia 73.1 ya wanafunzi waliofanya mtihani wa darasa la saba mwaka 2021 na wameingia kidato cha kwanza mwaka 2022.

“Utekelezaji wa mradi huo wanafunzi wote waliopangiwa kujiunga kidato cha kwanza mwaka 2022 hawakukabiliwa na changamoto ya uhaba wa vyumba vya madarasa ”.

Hata hivyo amesema mgao wa vyumba vya Madarasa katika Shule za Sekondari H ikiwemo Halmashauri ya Madaba vyumba 17 jumla ya shilingi milioni 340,Halmashauri ya Mbinga mgao wa vyumba vya Madarasa 88 zaidi ya Shilingi bilioni 1,Mbinga TC mgao wa vyumba vya Madarasa 34 Shilingi milioni 680.

Halmashauri ya Namtumbo vyumba vya Madarasa 80 zaidi ya Shilingi bilioni moja Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa vyumba vya mdarasa 44 ilighalimu shilingi milioni 880 ,Halmashauri ya Songea 46 shilingi milioni 920,Songea manispaa vyumba 26 Milioni 520,Tunduru 113 bil.mbili.



Moja ya madarasa ya UVIKO katika sekondari ya Kingerekiti Nyasa

## 2.WANAFUNZI RUVUMA WAMSHUKURU RAIS KWA SHULE ZA KISASA



WANANCHI mkoani Ruvuma wamemshukuru Rais Dkt.Samia Suluhu kwa kutoa fedha ambazo zimewezesha kujengwa kwa sekondari mpya zenye mazingira ya kuvutia katika Halmashauri zote nane.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga Grace Quietine amesema Rais ametoa shilingi milioni 470 kujenga sekondari mpya katika Kata ya Lusonga ambayo imekamilika kwa zaidi ya asilimia 90.

Amesema kiasi hicho cha fedha kimewezesha kujenga jengo la utawala,vyumba nane vya madarasa,maabara tatu,jengo la TEHAMA,jengo la maktaba,vyoo matundu 20 na sehemu ya kunawia maji mikono wanafunzi.

Amesema tayari wanafunzi wa kidato cha kwanza wamesajiriwa na kuanza masomo ambapo hivi sasa shughuli za umaliziaji zinaendelea zikiwemo za kuweka mfumo wa gesi na maji katika majengo ya maktaba na kwamba Halmashauri pia imeongeza fedha za kukamilisha mradi huo ambapo hadi sasa zaidi ya shilingi milioni 492 zimetumika.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya ya Tunduru Chiza Marando amesema anamshukuru Rais kwa upendeleo wa pekee wa kuwapatia kiasi cha shilingi bilioni 1.4 kujenga sekondari mpya tatu za

mfano katika wilaya hiyo ambazo zimekamilika na kuanza kuchukua wanafunzi wa kidato cha kwanza.

Amesema kila sekondari imepewa shilingi milioni 470 na kuzitaja sekondari hizo kuwa zimejengwa katika kata za Nakayaya,Majimaji na Lukumbule na kwamba kila shule imejenga jengo la utawala,madarasa nane,vyoo,samani,maabara tatu,jengo la TEHAMA na maktaba

“Shule zote tatu zinaendelea na hatua za ukamilishaji,lakini tumeshazisajiri na tumeshazifungua,wanafunzi wanaendelea kusoma, tunamshukuru sana Rais kwa kutumbuka Tunduru’’;alisema Marando.

Hata hivyo amesema kufunguliwa kwa shule hizo kumepunguza kero ya wanafunzi kwenye kata hizo kusafiri umbali mrefu kufuata sekondari.

Rais Samia pia ametoa shilingi milioni 470 kujenga sekondari mpya katika Kata ya Msisima Halmashauri ya Namtumbo na kwamba sekondari hiyo imefunguliwa na wanafunzi wameanza masomo.

Halmashauri nyingine ambazo zimepata fedha za ujenzi wa sekondari mpya ni Manispaa ya Songea katika Kata ya Mshangano zimetolewa shilingi milioni 470 kujenga sekondari ya Luhira.

Kata nyingine ni ya Amanimakoro Halmashauri ya Mbinga,Kata ya Riwundi wilaya ya Nyasa,Kata ya Lituta Halmashauri ya Madaba na Kata ya Kizuka Halmashauri ya wilaya ya Songea..



# SURA YA TATU

## UBORESHAJI ELIMU YA SEKONDARI TANZANIA

## 1. UJENZI WA SEKONDARI PROGRAM YA SEQUIP RUVUMA



Kwa mwaka 2021/2022 Mkoa ulipokea kiasi cha shilingi Bilioni **7,700,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya **11** za Sekondari katika Halmashauri zote 8 za Mkoa wa Ruvuma.ujenzi huu unajumuisha ujenzi wa shule ya Mkoa ya Wasichana inayojengwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo kwa gharama ya shilingi bilioni **3,000,000,000.00.** Ujenzi wa shule hizi upo katika hatua mbalimbali za ujenzi ikiwa ni maandalizi ya kupokea wanafunzi mwezi Januari 2023.

**Ukamilishaji wa Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa Maabara kupitia Fedha za Tozo na Serikali Kuu,**

Kwa mwaka 2021/2022 Mkoa ulipokea fedha kiasi cha Tshs. **2,152,500,000.00** kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba vya madarasa **128**

ya shule za Msingi na Sekondari na Maabara **23** za Shule za Sekondari kupitia fedha za Tozo na Serikali Kuu. Pia tulipokea Tshs. **540,000,000.00** kwa ajili ya ujenzi wa Madarasa na mabweni Shule Sekondari ya Wasichana Songea na Shule ya Sekondari ya Wavulana Songea



Baadhi ya vyumba vya madarasa yaliyojengwa katika sekondari mpya ya Luhira Kata ya Mshangano Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma kupitia Programu ya Uboreshaji Elimu ya Sekondari SEQUIP



## 2.SEKONDARI MPYA HALMASHAURI YA WILAYA YA MBINGA ILIYOJENGWA KUPITIA PROGRAM YA SEQUIP




SERIKALI imetoa Sh.milioni 470 kujenga shule mpya ya sekondari katika kijiji cha Amani-Makolo kata ya Amani-Makolo Halmashauri ya wilaya Mbinga mkoani Ruvuma, ili kumaliza kero ya wanafunzi wanaotoka katika kata hiyo kwenda kata ya Mkako umbali wa km 15 kufuata masomo

Awali wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi katika kata hiyo na kuchaguliwa kuendelea na kidato cha kwanza walilazimika kwenda kata

nyingine kama vile Mkako,Rwanda na wengine hata shule zilizopo Mbinga mjini kwa ajili ya kuanza masomo ya sekondari.

Kaimu Afisa elimu sekondari wa Halmashauri hiyo Rashid Bundala amesema,kujengwa kwa shule hiyo ni ukombozi mkubwa hata kwa wazazi ambao walilazimika kuwalipia watoto wao gharama ya kusafiri kwenda shule na kurudi nyumbani kila siku.

Amesema,baadhi ya wanafunzi wanaotoka vijiji vya kata hiyo walilazimika kupanga vyumba uraini na kuanza kujitegemea licha ya umri mdogo walionao

Bundala alieleza kuwa,kutokana na changamoto hiyo baadhi ya watoto hasa wa kike walishawishika kuanza mahusiano ya kimapenzi na watu wazima wasiokuwa na maadili mema na hatimaye kushindwa kumaliza masomo kwa kupata mimba na wengine kuchoshwa na umbali uliopo.

Aidha amesema,ujenzi wa shule ya Sekondari Mndeme ni utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi inayotaka kila kata kuwa na shule ya sekondari ili vijana wengi wanaomaliza darasa la saba wapate nafasi ya kuendelea na elimu ya sekondari.

Amemshukuru Rais Dkt Samia Suluhu Hassan,kutoa fedha ili kujenga shule hiyo sekondari ambayo ni msaada mkubwa kwa watoto wa kata ya Amani-Makolo ambao sasa wanatoka nyumbani na kwenda shule iliyopo karibu na makazi yao.

Baadhi ya wanafunzi wa shule ya sekondari ya Mndeme,wameishukuru serikali kuwajengea shule mpya na kuwaondolea adha ya kutembea umbali mrefu kwenda katika kata nyingine kufuata masomo.

Solana Adam amesema,wanafunzi wanaotoka katika kijiji hicho walikuwa wakitembea umbali wa kilomita 15 kila siku kwenda na kurudi hadi shule ya sekondari Mkako na kufika wakiwa wamechoka,lakini kwa kujengewa shule hiyo karibu itawafanya kusoma kwa bidii.

Ameiomba serikali kuwajengea mabweni ili wanafunzi hususani wa kike waweze kuishi shuleni ili wapate muda mwingi wa kusoma,badala ya kurudi nyumbani ambako wanakutana na kazi nyingi zinazowakosesha kupata muda wa kujisomea.

Hadija Mustapha amesema changamoto kubwa ni maji safi na salama,kwani licha ya kuwepo kwa mtandao wa maji lakini yanayotoka hayafai kwa matumizi ya binadamu kwa kuwa yanatope jingi hivyo wanalazimika kutumia maji ya mvua yanatoka juu ya bati za nyumba

Ujenzi wa madarasa kupitia program ya SEQUIP



Miongoni mwa majengo sekondari mpya katika Halmashauri ya wilaya ya Mbinga



## 3.SEKONDARI MPYA YA WASICHANA MKOANI RUVUMA




***Pichani sekondari ya wasichana ya Dkt.Samia Suluhu Hassan iliyojengwa wilayani Namtumbo***

Serikali kupitia program ya SEQUP imetoa shilingi bilioni tatu kujenga sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Ruvuma kwa lengo la kuweka

kwenye elimu ya mtoto wa kike ili kumpunguzia changamoto zinazowakabili

Sekondari hiyo ya Wasichana mkoani Ruvuma imejengwa eneo la Migelegele Kata ya Lwinga Wilaya ya Namtumbo na kupewa jina shule ya sekondari ya wasichana ya Dk Samia Suluhu, ambapo itakapokamilika itapokea wanafunzi zaidi ya 1000 na inatarajia kuanza Julai 202

## 4.BILIONI 20 ZILIVYOJENGA SHULE MPYA 11 NA MADARASA 656 MKOANI RUVUMA



RAIS Dkt Samia Suluhu Hassan ametoa zaidi ya shilingi bilioni 20 kujenga sekondari mpya 11 na vyumba vya madarasa 656 katika Mkoa wa Ruvuma.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas amesema kati ya fedha hizo zaidi ya shilingi bilioni 10 zilitolewa kupitia UVIKO ambazo zimejenga madarasa 500,shilingi bilioni 7.7 zimejenga shule mpya za sekondari 11 kupitia program ya SEQUIP na shilingi bilioni 3.1 zimejenga madarasa 156 katika shule za sekondari mkoani Ruvuma.

“Serikali imetekeleza wajibu wake kilichobaki ni wajibu wa wazazi kuhakikisha watoto wao wanahudhuria shule “,alisisitiza Kanali Thomas.

## 5.SEKONDARI MPYA YA LUHIRA SONGEA INAVYOVUTIA WANAFUNZI NA WALIMU



**J**engo la Utawala katika sekondari mpya ya Luhira kata ya Mshangano Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma ambapo serikali ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kupitia program ya uboreshaji Elimu ya Sekondari (SEQUIP) imetoa shilingi milioni 470 kutekeleza mradi huo

## 6.MAZINGIRA RAFIKI YA KUSOMEA WANAFUNZI MBINGA



Jengo la Utawala katika sekondari mpya ya Lusonga kata ya Lusonga Halmashauri ya Mji wa Mbinga mkoani Ruvuma ambapo serikali ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kupitia program ya uboreshaji Elimu ya Sekondari (SEQUIP) imetoa shilingi milioni 470 kutekeleza mradi huo



## 7.HALMASHAURI SONGEA WANAVYOJINUA SEKONDARI YA KIZUKA



Pichani ni jengo la Utawala katika sekondari mpya ya Kizuka Kata ya Kizuka Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma ambapo serikali ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kupitia program ya uboreshaji Elimu ya Sekondari (SEQUIP) imetoa shilingi milioni 470 kutekeleza mradi huo



## 8.SEKONDARI MPYA YA JOSEPH KIZITO KIVUTIO CHA WANAFUNZI




Sekondari mpya ya Kata ya Lituta Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma iliyogharimu shilingi 470.

mradi huu umetekelezwa na serikali kupitia program ya Uboreshaji Elimu ya Sekondari (SEQUIP) ambapo katika Mkoa wa Ruvuma kupitia program hiyo zimejengwa sekondari mpya 11 kwa gharama ya shilingi bilioni 7.7

## 9.SEKONDARI TATU ZA MFANO ZILIZOJENGWA TUNDURU




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan ametoa shilingi bilioni 1.4 kujenga sekondari mpya tatu katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma.Mkurugenzi Mtendaji wa

Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Chiza Marando amezitaja shule hizo kuwa zimejengwa katika kata za Nakayaya,Majimaji na Lukumbule na kwamba kila shule imegharimu shilingi milioni 470.Amesema shule hizo zimesajiriwa na kuanza kuchukua wanafunzi .



Moja ya madarasa ya kisasa katika shule mpya ya sekondari Kata ya Majimaji wilayani Tunduru mkoani Ruvuma ambapo serikali imetoa shilingi milioni 470 kujenga shule hiyo



Moja ya madarasa katika sekondari Kata ya Nakayaya wilayani Tunduru ambayo serikali imetoa shilingi milioni 470 kutekeleza mradi huu

## 10.TUNDURU WANAVYOJIVUNIA SEKONDARI MPYA



Sekondari mpya ya Kungu kata ya Nakayaya Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru ni miongoni mwa sekondari mpya 11 zilizojengwa mkoani Ruvuma.na serikali ya Awamu ya Sita kupitia program ya Uboreshaji Elimu ya Sekondari (SEQUIP).Sekondari hii yenye mazingira ya kuvutia imegharimu shilingi milioni 470



Jengo la utawala katika sekondari mpya Kata ya Nakayaya wilayani Tunduru mkoani Ruvuma ambayo serikali ya Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan imetoa shilingi milioni 470 kutekeleza mradi



## 11.SEKONDARI MPYA YA MSISIMA NAMTUMBO



Sekondari mpya ya Msisima imejengwa kilometa 150 toka makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma.Serikali imetoa shilingi milioni 470 kupitia program ya Uboreshaji Elimu ya Sekondari (SEQUIP) kutekeleza mradi huu

## 12.MRADI WA SEKONDARI YA MFANO WA MAJIMAJI



Mradi wa shule mpya ya sekondari ya Majimaji Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma,serikali imetoa shilingi milioni 470 kutekeleza mradi huo

## 13.SERIKALI YATOA BILIONI 1.4 KUJENGA SEKONDARI TATU ZA MFANO TUNDURU



SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan imetoa shilingi bilioni 1.4 kujenga shule mpya tatu za sekondari katika wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma.

Akizungumza wakati wa ukaguzi wa shule hizo uliofanywa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas,Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Tunduru Dkt.Julius Lingu amezitaja shule hizo kuwa ni Nakayaya,Majimaji na Lumbukule.

Amesema shule hizo zinajengwa kupitia Programu ya Uboreshaji Elimu ya Sekondari nchini (SEQUIP) ambapo kila shule imepewa shilingi milioni 470 kutekeleza mradi huo.

“Ujenzi wa shule hizo bado unaendelea,kuna mapungufu ambayo yamejitokeza katika ukaguzi uliofanywa na Mkuu wa Mkoa hivyo mapungufu hayo yatafanyiwa kazi na kufanyiwa marekebisho ili shule hizo ziweze kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza ifikapo Januari 2023’’,alisisitiza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Tunduru Chiza Marando ameyataja majengo yanayojengwa katika kila shule kuwa ni ujenzi wa

maabara tatu,vyumba nane vya madarasa,matundu 20 ya vyoo,jengo la utawala,minara miwili ya maji,jengo la TEHAMA na jengo la maktaba.

Akizungumza mara baada ya kukagua shule hizo,Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas amemshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa shilingi bilioni 7.7 kutekeleza ujenzi wa shule mpya 11 za sekondari mkoani Ruvuma.

Kati ya shule hizo mpya, shule tatu zinajengwa katika wilaya ya Tunduru hivyo RC Thomas amemuagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo kusimamia ujenzi wa shule hizo na kuweka samani zake katika kila darasa ili shule hizo zianze kuchukua wanafunzi Januari 2023.

“Mhe.Rais alishamaliza kazi yake ya kututafutia pesa kutuletea hivyo ni wajibu wetu sisi sote kama timu kusimamia na kuhakikisha miradi ya serikali inatekelezwa kwa viwango na thamani inayolingana na fedha’’,alisisitiza.

Serikali Kuu kupitia Programu ya Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari nchini (SEQUIP) inajenga shule mpya za sekondari 1000 katika nchi nzima,kati ya hizo shule 11 zinajengwa katika Mkoa wa Ruvuma.



Jengo la utawala katika sekondari mpya ya Kata ya Nakayaya wilayani Tunduru ambapo serikali imetoa shilingi milioni 470 kutekeleza mradi huu

## 14.SEKONDARI YA MFANO KATA YA KIZUKA SONGEA



SERIKALI ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imetoa shilingi milioni 720 kuanzisha shule mpya mbili katika Halmashauri ya wilaya ya Songea mkoani Ruvuma

Mkurugenzi wa Halmashari ya Wilaya ya Songea Neema Maghembe amezitaja shule hizo kuwa ni shule ya sekondari Kizuka katika Kata ya Kizuka ambayo serikali imetoa shilingi milioni 470 kutekeleza mradi huo.

Ameyataja majengo ambayo yanajengwa katika sekondari hiyo kupitia fedha za serikali za SEQUIP kuwa ni vyumba vinne vya madarasa,jengo la utawala,maktaba, vyoo na jengo la TEHAMA.

Amesema utekelezaji wa mradi huo hadi sasa umefikia asilimia 95 na kwamba shule inatarajia kuanza kuchukuwa wanafunzi kuanzia Januari 2023.

Mkurugenzi huyo pia ameitaja shule tarajiwa ya msingi inayojengwa katika kitongoji cha Lizaboni Kata ya Muhukuru iliyopo kilometa 140 kutoka mjini Songea ambayo serikali imetoa shilingi milioni 250 kutekeleza mradi huo.

“Mradi huu unatekelezwa na fedha kutoka serikali kuu kiasi cha shilingi milioni 250 ambazo zinajenga jengo la utawala,vyumba tisa vya madarasa na samani zake na vyoo matundu 30’’,alisema Maghembe.

Hata hivyo amesema mradi upo katika hatua za awali za utekelezaji na kwamba mradi unatarajiwa kukamilika Desemba 30 mwaka huu ambapo Januari mwakani shule inatarajia kuanza kuchukua wanafunzi.

Akizungumza baada ya kukagua miradi hiyo Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Stephen Ndaki,ameipongeza Halmashauri hiyo kwa usimamizi unaofanywa kwenye miradi,hata hivyo ameagiza kuwa na mpango kazi wa kutembelea na kukagua miradi katika ngazi ya Halmashauri ili miradi iweze kutekelezwa kwa ubora na kwa wakati.

Ameagiza usimamizi unaofanywa kwenye miradi uheshimu kanuni za utawala bora,uwazi na ushirikishwaji na kwamba Halmashauri zijitahidi kuzijengea uwezo Kamati za Ujenzi ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na tija.

# SURA YA NNE

## UJENZI WA MADARASA YA SEKONDARI MKOANI RUVUMA

### 1.SERIKALI YATOA BILIONI 3.2 KUJENGA MADARASA MAPYA MKOANI RUVUMA



Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan imetoa shilingi bilioni 3.12 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 156 mkoani Ruvuma.

Hayo yamesemwa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas kwenye ukumbi wa Manispaa ya Songea katika kikao kazi cha maelekezo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza Januari 2023.

Akizungumza kwenye kikao hicho kilichowashirikisha watendaji ngazi ya Mkoa na wilaya zote za Mkoa wa Ruvuma,Kanali Thomas amempongeza Rais kwa jitihada zake za kuhakikisha anaondoa tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa katika shule za sekondari.

“kwa mara nyingine tena Mkoa wetu umepokea shilingi bilioni 3.12 kutoka kwa Mhe.Rais kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 156 katika

shule za sekondari,ujenzi unatakiwa kukamilika Desemba 15,2022 ambayo ni sawa na siku 75 tu hivyo hatuna budi kufanya kazi usiku na mchana'',alisisitiza Kanali Thomas.

Ili kuhakikisha majengo hayo yanakamilika kwa wakati,Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma ameagiza wilaya zote kuimarisha dhana ya ushirikishwaji na uwajibikaji,Halmashauri zote kuunda kamati za usimamizi wa miradi na kuanza mchakato wa manunuzi ya vifaa na upatikanaji wa mafundi wenye uwezo.

Hata hivyo Mkuu wa Mkoa ameagiza usimamizi na ufuatiliaji wa ngazi zote ufanyike ili kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa wakati na kwa ubora.

Akizungumza kwenye kikao hicho Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Stephen Ndaki amesema Mkoa wa Ruvuma kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa TAMISEMI umepokea kiasi cha shilingi bilioni 3.12 kutoka serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 156 katika shule za sekondari 68.

Ameyataja maelezo mahususi ya utekelezaji wa mradi huo kuwa ni kufuata mwongozo wa force account katika utekelezaji wa mradi na kutumia ramani ya darasa iliyoelekezwa kwenye program EP4R na UVIKO 19.

Maelekezo mengine ameyataja kuwa ni kuhakikisha ujenzi unakamilika ifikapo Desemba 15,2022 na utekelezaji wa miradi yote uzingatie thamani ya fedha na ubora wa miradi.

Naye Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Ruvuma anayeshughulikia Mipango Jumanne Mwankoo amebainisha kuwa kati ya shilingi bilioni 3.12 zilizotolewa,Manispaa ya Songea imepokea shilingi bilioni 1.52 kwa ajili ya kujenga vyumba 76 vya madarasa.

Mwankoo ameitaja Halmashauri ya Mbinga Mji kuwa imepokea shilingi milioni 220 kwa ajili ya kujenga vyumba vya madarasa 11,Halmashauri ya Namtumbo imepokea shilingi milioni 340 kwa ajili ya kujenga madarasa 17 na Halmashauri ya Nyasa imepokea sh. Milioni 240 kwa ajili ya kujenga madarasa 12.

## 2.BILIONI 3.2 ZILIVYOJENGA MADARASA MAPYA 156 KATIKA SHULE ZA SEKONDARI MKOANI RUVUMA



SERIKALI mkoani Ruvuma imekamilisha mradi wa ujenzi wa madarasa 156 pamoja na samani zake katika shule za sekondari yaliyogharimu shilingi bilioni 3.1.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas amesema serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan mwezi Oktoba mwaka 2022 ilitoa fedha za kutekeleza mradi huo mkoani Ruvuma.

“Madarasa yapo tayari kupokea wanafunzi waliochaguliwa kidato cha kwanza Januari 2023”,alisisitiza RC Thomas.

Hata hivyo amesema hayo ni mafanikio makubwa kwa kuwa sasa katika Mkoa mzima shule zote za sekondari za Serikali zina uhakika wa kupokea wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na shule hizo.

Amesema hakuna kikwazo tena cha uhaba wa vyumba vya madarasa hivyo ametoa rai kwa wazazi na walezi kuhakikisha watoto wao wanaripoti bila kukosa.

Katika hatua nyingine Mkuu wa Mkoa amemshukuru Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutoa shilingi bilioni 7.7 zilizojenga shule mpya za sekondari 11 mkoani Ruvuma katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022. Amesema uboreshaji wa miundombinu ya elimu umepunguza utoro na kuongeza ufaulu.

Ametolea mfano ufaulu wa mitihani ya Taifa ya kidato cha nne mwaka 2021 Mkoa ulikuwa na ufaulu wa asilimia 90.1.

Kulingana na RC Thomas matokeo ya mitihani ya Taifa ya kidato cha sita mwaka 2022 Mkoa wa Ruvuma umefaulisha kwa asilimia 99.9.

Hata hivyo amesema jitihada zinafanyika kuboresha ufaulu wa darasa la saba na kidato cha nne.



**Moja ya madarasa katika shule ya sekondari ya Dkt.Samia Namtumbo**

## 3.WANAFUNZI MBINGA GIRLS WAMSHUKURU RAIS SAMIA




WANAFUNZI wa shule ya sekondari ya wasichana Mbinga wamesema,kujengwa kwa vyumba vipya vya madarasa vimewaongezea ari ya kujisomea na kuhaidi watavitumia kusoma kwa bidii ili waweze kufanya vizuri katika masomo yao.

Wameishukuru serikali kuwajengea vyumba vipya vya madarasa ambavyo vimesaidia kupunguza msongamano na kuongeza utulivu madarasani wakati wa kujisomea.

Wamesema hayo  wakati wakizungumza, juu ya ujenzi wa  miumbombinu ya elimu iliyotekelezwa na serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan  katika kipindi cha miaka miwili cha uongozi wake.

“tunamshukuru sana mama yetu Rais Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutujengea vyumba vipya vya madarasa na mabweni katika shule yetu,kwa sasa tunasoma kwa amani na utulivu mkubwa,hapo awali wenzetu waliotangulia katika shule hii walikutana na changamoto kubwa ya msongamano darasani ambao sasa haupo tena”alisema mwanafunzi wa kidato cha nne Uwezo Komba.

Komba alieleza kuwa,ujenzi wa madarasa mapya sambamba na viti na meza umehamasisha hata wanafunzi wanaopelekwa katika shule hiyo kufurahi mazingira mazuri na kupenda shule tofauti  na hapo awali ambapo wazazi walilazimika kwenda na vifaa ambavyo sasa mwanafunzi anavikuta shuleni.

Debora Mapunda amesema,tangu walipofika katika  shule hiyo wamefurahia mazingira ya shule kutokana na uwekezaji mkubwa wa miundombinu uliofanywa na serikali ya awamu ya sita na kuhaidi kuitunza ili iweze kudumu kwa muda mrefu.

Nuru Ibrahim mwanafunzi wa kidato cha nne amesema,kabla ya ujenzi wa vyumba vipya vya madarasa kero kubwa ilikuwa ni msongamano wa wanafunzi kwani darasa moja lilikuwa na wanafunzi kati ya 40 na 45,hivyo kukosa na utulivu na kushindwa kusikiliza yanayofundishwa na walimu.

Aidha,ameishauri serikali kuendelea kuwekeza kwenye  ujenzi wa mabweni na kujenga wigo(uzio) kuzunguka eneo lote la shule  na viwanja vya michezo ili waweze kushiriki michezo mbalimbali hasa ikizingatiwa kuwa kwa sasa michezo ni ajira.

Kwa upande wake Mkuu wa shule hiyo Theresia Mlwilo, ameishukuru serikali kwa kutoa jumla ya shilingi milioni 40  kwa ajili ya kujenga vyumba viwili vya madarasa ambavyo vimesaidia sana wanafunzi kuwa na sehemu nzuri ya kujifunzia na walimu kufundishia.



**Serikali imeboresha miundominu ya kusomea wanafunzi Ruvuma**

## 4.MAKITA SEKONDARI WAMSHUKURU RAIS KWA KUWAJENGEA MADARASA



WANAFUNZI wa shule ya Sekondari Makita Halmashauri ya mji Mbinga mkoani Ruvuma,wameishukuru serikali kuwajengea vyumba vipya vya madarasa na kupunguza msongamano mkubwa wa wanafunzi madarasani hivyo kuwasaidia kusoma katika mazingira mazuri.

Wamesema,wamefurahishwa na mpango wa serikali ya awamu ya sita kutokana na mkakati wake wa kuboresha na kuweka mazingira mazuri ya kujifunzia kwa wanafunzi na walimu kufundishia ikiwamo vyumba vipya vya madarasa,meza,viti na ofisi za walimu.

Pius Komba mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule hiyo amesema,kutokana na uwekezaji huo wa serikali watahakikisha wanasoma kwa bidii na kufanya vyema katika masomo yao na hatimaye waweze kutimiza malengo yaliyowaleta shuleni.

Komba,amewaomba wazazi ambao bado hawajapeleka watoto wao shule,kuhakikisha wanawapeleka haraka ili wakapate haki yao ya elimu kwani muda wa masomo umeshaanza na wao wamebaki nyumbani.

Aidha,amemshukuru Mkuu wa shule hiyo Mwalimu Emanuel Mwamasika kwa kukubali kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza hata wale

wasiokuwa na mahitaji muhimu jambo linalowapa hamasa ya kusoma kwa bidii.

Happy Kinyunyu amesema,madarasa mapya yaliyojengwa kwa ubora yanawafanya wanafunzi kupenda shule,kusoma kwa bidii na kuwa wasikivu darasani ikilinganishwa na hapo awali kwa kuwa hakuna changamoto zinazoweza kuwakatisha tamaa.

Amewaasa wanafunzi wenzake wa kike,kusoma kwa bidii ili kutimiza malengo yao badala ya kujiingiza katika ulevi,uesharati na kufanya kazi za nyumbani(House Girls) tabia iliyopelekea baadhi ya watoto wa kike kushindwa kutumiza malengo yao.

Kwa upande wake Mkuu wa shule hiyo Emanuel Mwamasika amesema,walipokea kiasi cha Sh.milioni 40 ambazo zimefanikisha kujenga vyumba vipya viwili vya madarasa.

Amesema hapo awali kulikuwa na uhaba mkubwa wa madarasa,lakini baada ya kupata fedha hizo na kujenga vyumba vipya sasa wanafunzi wanakaa madarasani kwa nafasi na hakuna aliyekosa meza na kiti na wana ziada ya chumba kimoja.

Mwamasika,ameipongeza serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kutekeleza kwa vitendo Ilani yake jambo lililosaidia kuwa na mazingira mazuri na rafiki katika sekta ya elimu hapa nchini.

Mwamasika amesema,shule hiyo imepangiwa kupokea wanafunzi 332 wa kidato cha kwanza.



# 5.SONGEA WAKABIDHI VYUMBA VYA MADARASA 76



Vyumba vya madarasa 76 vilivyogharimu shilingi bilioni 1.5 katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma vimekamilika na kukabidhiwa kwa uongozi wa Wilaya ya Songea tayari kwa matumizi ya wanafunzi wa kidato cha kwanza.

## 6.HALMASHAURI TATU SONGEA ZAKABIDHI MADARASA 96



Mkuu wa Wilaya ya Songea Mheshimiwa Pololet Mgema amesema Halmashauri tatu katika Wilaya ya Songea zimekamilisha kwa mafanikio makubwa kazi ya kujenga madarasa 96 ya Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mgema amesema hayo baada ya kukagua madarasa 29 kati ya 76 yaliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

“Sisi Wilaya ya Songea tumekwishafanya kazi tuliotumwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan tumeikamilisha kwa mafanikio makubwa “,alisema

na kuongeza kuwa wanafunzi wote watakaojiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023 watapata mahali pazuri pa kusomea.

Amesema madarasa yote 96 yaliyojengwa Wilaya ya Songea kwa gharama ya shilingi bilioni 1.9 .



## SURA YA TANO

## UTEKELEZAJI WA MRADI WA BOOST TANZANIA

### 1.MRADI WA BOOST KUJENGA MADARASA 12,000,SHULE SALAMA 6,000



WATAALAM zaidi ya 280 kutoka ngazi za Halmashauri na mikoa ya Ruvuma,Njombe na Iringa  wamepata mafunzo elekezi ya timu za utekelezaji wa mradi wa Kuimarisha Ujifunzaji katika Elimu ya Awali na Msingi (BOOST) unaogharimu sh.trilioni 1.15 wenye lengo la kujenga madarasa 12,000 na shule salama 6,000 katika nchi nzima.

Mafunzo hayo ambayo yameandaliwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI yamefanyika kwa siku mbili katika shule ya sekondari Lugalo Manispaa ya Iringa.

Akizungumza wakati anafungua mafunzo hayo,Mratibu wa Mafunzo kutoka Idara ya Usimamizi wa Elimu Ofisi ya Rais TAMISEMI Yusuph Singo amesema TAMISEMI imeandaa mafunzo hayo katika Kanda tisa kwa lengo la kuwajengea uwezo wajumbe wa timu hizo kuhusu usimamizi wa mradi wa BOOST.

Amezitaja timu hizo kuwa zinaundwa na wajumbe 12 kutoka ngazi ya Halmashauri ambao ni Afisa Elimu Msingi,Afisa Maendeleo ya

Jamii,Mhandisi,Mwalimu Mkuu,Afisa Manunuzi,Mthibiti Ubora wa Shule, Afisa Ustawi wa Jamii,Afisa Elimu Kata,Afisa Mipango,Afisa Habari na Mratibu wa Mradi.

Amesema katika ngazi ya Mkoa timu inaundwa na wajumbe wanane ambao ni Afisa Elimu Mkoa,Mratibu wa Mradi wa BOOST,Mhandisi,Afisa Habari,Afisa Maendeleo ya Jamii,Afisa Ustawi wa Jamii,Afisa Mipango na Mdhibiti Ubora wa Shule Kanda.

“Mheshimiwa Rais ametafuta fedha kiasi cha shilingi Trilioni 1.15 kwa ajili ya uboreshaji mkubwa wa elimu kupitia Mradi wa kuimarisha ujifunzaji shule za msingi na awali, utekelezaji wa mradi huu ni wa miaka mitano utaboresha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji, ujuzi na ubora wa walimu katika ufundishaji’’,alisisitiza Singo.

Amesema mradi utatekelezwa katika afua mbalimbali ikiwemo kuboresha miundombinu ya shule za msingi kwa kuzingatia mahitaji hususan ujenzi wa madarasa, uimarishaji wa mpango wa shule salama, kuimarisha uwiano wa uandikishwaji wa wanafunzi wa elimu ya awali, kuboresha vifaa na njia za ufundishaji elimu ya awali, pamoja na kuimarisha na kuendeleza mpango wa mafunzo ya walimu kazini.

Mratibu huyo wa Mafunzo wa TAMISEMI amesema katika kipindi cha miaka mitano madarasa 12,000 yatajengwa nchi nzima katika shule za msingi kupitia mradi wa BOOST na kwamba kwa kila mwaka yanatarajiwa kujengwa madarasa 3,000 ambapo afua zote zitatekelezwa kwa utaratibu wa lipa kulingana na matokeo(EP4R).

Hata hivyo amesema kupitia mradi wa BOOST shule za msingi 800 zinatarajiwa kuwekewa vifaa vya TEHAMA ili kuwawezesha walimu kujifunza utoaji wa elimu endelevu hivyo kuboresha elimu ya msingi.

Kwa upande wake Mratibu wa Mpango wa Shule Salama kitaifa Hilda Mgomapayo amesema kupitia mradi wa BOOST shule salama 6,000 zinatarajiwa kujengwa katika nchi nzima katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa mradi huu ambapo katika awamu ya kwanza zinatarajiwa kujengwa shule 1000.

Amesema shule salama zitawajengea uwezo wanafunzi kujiamini katika mfumo wa elimu,kuimarisha stadi za Maisha,mawasiliano na mahusiano hivyo Watoto kufikia malengo yao.

Kwa upande wake Mwezeshaji kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI Lugalata Mwshemi akizungumzia afua ya kuongeza uandikishaji Watoto wa

awali,amesema kupitia mradi wa BOOST inatarajiwa kuboresha, uandikisha wa wanafunzi elimu ya awali kwa kuongeza idadi ya wanafunzi katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji.

Amesema katika utekelezaji wa mwaka wa kwanza uandikishaji wa elimu ya awali 2021/2022 unatarajiwa kuwa ni asilimia 75,mwaka 2022/2023 asilimia 80.14,mwaka 2023/204 asilimia 81.76,mwaka 2024/2025 asilimia 83.38 na mwaka 2025/2026 kuwa asilimia 85.

Hata hivyo amesema lengo ni kuhamasisha jamii kuhusu uandikishaji wanafunzi wa awali wenye umri wa kati ya miaka mitatu hadi mitano na kuhakikisha wanafunzi wote waliondikishwa wanakamilisha mafunzo kwa mwaka mmoja.

Takwimu zinaonesha kuwa hapa nchini kuna shule za msingi zaidi ya 17,000,hata hivyo kupitia mradi wa Kuimarisha Ujifunzaji katika Elimu ya Awali na Msingi (BOOST) watoto zaidi ya milioni 12 wanatarajia kunufaika na mradi huo.



**Moja ya madarasa yenye miundombinu bora inayofaa kwa wanafunzi wa shule za msingi**

**2.MRADI WA KUBORESHA MIUNDOMBINU YA SHULE ZA MSINGI BOOST MKOANI RUVUMA**



*Pichani ni washiriki wa mafunzo ya Mradi wa Kuimarisha Ujifunzaji wa Elimu ya Awali na Msingi (BOOST) yaliyoshirikisha*

*wataalam zaidi ya 280 kutoka mikoa ya Ruvuma Iringa na Njombe.*

Ofisi ya Rais - TAMISEMI imekamilisha uchambuzi wa tathimini ya mahitaji na hali ya Miundombinu ya Shule za Msingi katika Halmashauri zote **104** nchini ambayo ilifanyika kwa kipindi

cha mwezi Julai hadi Disemba, 2022 Kutokana na tathimini hiyo, kwa mwaka 2022123 Mkoa wa Ruvuma umepatiwa Jumla ya Shilingi **7,291,500,000** kwa ajili ya ujenzi wa-Shule mpya za Msingi **12**, vyumba vya madararasa **85** vya Shule za Msingi, vyumba vya Madarasa ya'mfano ya Elimu ya Awali **16**, matundu ya vyoo **111**, na nyumba za walimu **02** (2 in 1).

Mradi huu unakwenda kutekelezwa katika halmashauri zote **8** za mkoa wa Ruvuma kwa vipengele vyote vilivyo tajwa hapo juu kwa kuzingatia mahitaji ya halmashauri husika.kwa hiyo kiwango cha fedha katika Halmashuri kitatofautiana kutoka halmashauri moja na nyingine kwa maeneo yaliyoainioswa hapo juu kama yafuatayo;-Idadi za shule zitakazo pokee fedha katika Halmashauri,vvyumba vya madarasa vitakavyo jengwa,vyumba vya madarasa vya mfano Elimu ya Awali,Matundu ya vyoo, na Nyumba za walimu.

**MCHANGANUO WA MGAO WA FEDHA ZA UJENZI WA MIUNDOMBINU KWA KILA HALMASHAURI KWA KUPITIA MRADI BOOST**

| NA | HALMASHAURI | IODADI YA SHULE | IDADI YA MIRADI | JUMALA YA FEDHA ZIOLIZOTOLEWA |
|---|---|---|---|---|
| 2 | MADABA | 6 | 23 | 610,300,000 |
| 3 | MBINGA | 7 | 28 | 663,400,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4 | MBINGA TC | 8 | 29 | 995,000,000 |
| 5 | NAMTUMBO | 9 | 31 | 1,445,600,000 |
| 6 | NYASA | 5 | 22 | 724,200,000 |
| 7 | SONGEA | 7 | 31 | 735,400,000 |
| 8 | SONGEA MC | 7 | 30 | 893,000,000 |
| 8 | TUNDURU | 7 | 31 | 1,224,600,000 |
| **JUMLA** | | 56 | 226 | 7,291,500,000 |




Mradi wa madarasa mapya ya awali katika shule ya msingi Mbulani Kata ya Ruvuma Manispaa ya Songea ambapo serikali imetoa shilingi milioni 43 kujenga madarasa hayo ya kisasa ambapo serikali pia kupitia mradi wa BOOST inatarajia kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya msingi Mbulani na kutoa fedha za kukarabati majengo ya shule ya msingi Mbulani inayotumika sasa.

## 3.UJENZI WA MADARASA MAPYA KATIKA SHULE YA MSINGI




MRADI wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa katika shule ya Msingi Liweta na mradi wa chumba kimoja cha darasa shule ya sekondari Lupunga Kata ya Mpandangindo Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

Kamati ya Siasa ya CCM Mkoa wa Ruvuma ikiongozwa na Mwenyekiti wake Komred Odo Mwisho imetembelea na kukagua miradi ya madarasa na kuridhishwa na ubora wa madarasa hayo ambayo yanapunguza uhaba wa vyumba vya madarasa katika shule hizo.

## SURA YA SITA

## UKARABATI SEKONDARI KONGWE MKOANI RUVUMA

### I.UKARABATI SEKONDARI YA WAVULANA SONGEA



SERIKALI imetoa zaidi ya Millioni 952,katika shule ya Sekondari ya wavulana Songea iliyopo katika Manispaa ya Songea Mkoani Ruvuma kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa Majengo na miundombinu yake.

Akitoa taarifa kwa wajumbe wa kamati ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliotembelea shule hiyo j, Mkuu wa shule hiyo John Sweke,amesema ukarabati wa shule hiyo unatarajia kukamilika ndani ya siku 30.

Ameyataja Majengo yanayokarabatiwa kuwa ni Nyumba tatu za Waalimu,Mabweni 19,Maabara tatu,Kumbi tatu za mihadhira,Jengo la utawala,Zahanati,Stoo,Madarasa 24,Karakana,na Nyumba nne za vyoo na mabafu.

Amesema miundombinu ya shule hiyo imekusudiwa kukidhi wanafunzi 120 na kwamba Mwaka 1956 ilianzisha tahasusi ya HGL ambapo hadi sasa shule hiyo ina tahasusi za masomo ya PCM,PCB,PGM,CBG,EGM na HGE.

“Shule hii mwaka huu imeteuliwa kuwa moja ya shule zenye kutoa elimu jumuishi hapa nchini, kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza wa kawaida na wenye mahitaji maalimu ili kusoma kwa pamoja’’,alisema Sweke.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo wa shule,Ufaulu kwa kidato cha pili kwa miaka mitano mfululizo ulikuwa ni asilimia 97, kidato cha nne ni asilimia 97.5 na ufaulu kidacho cha sita ni asilimia 98.5.

Shule ya sekondari ya wavulana Songea ilianzishwa mwaka 1950 ambapo hivi sasa, ina jumla ya Wanafunzi 798,walimu 52,wapishi wawili,Mlinzi mmoja,Mhasibu mmoja,Boharia mmoja,wafunzi wenye ulemavu tofauti 40 na walimu wenye utaalamu wa elimu maalumu ni 11.

Wajumbe wa Kamati ya siasa wa Mkoa wa Ruvuma wametoa pongezi kwa Mkuu wa shule wa Sekondari ya Wavulana Songea kwa kusimamia ukarabati wa majengo katika kipindi cha mwezi mmoja.

Mkuu wa shule hiyo John Sweke akizungumza na wajumbe wa CCM wa Mkoa na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma waliotembelea katika shule hiyo amesema shule ilipokea fedha kutoka ofisi ya TAMISEMI kiasi cha zaidi ya shilingi milioni 952 kwa ajili ya ukarabati wa majengo na miundombinu

Amesema. taratibu za ukarabati ulianza tarehe 09/05/2019 na kwamba ukarabati wa majengo na miundombinu yake umefanyika kwa kutumia force account na mradi umegharimu kiasi cha Tshs. 872,417,048.00 na umefikia asilimia 98 ya ukamilishaji na wamebakiwa na akiba ya Tshs. 80,000,000 ambazo zinaendelea na ukarabati wa maeneo yasiyofanyiwa ukarabati.

Kulingana na Sweke ,Maeneo yaliyofanyiwa kazi ni ukarabati wa vyumba vya madarasa 24, ukarabati wa mabweni 21, ukarabati wa majengo ya maabara matatu, ukarabati wa kumbi nne, ukarabati wa jengo la utawala, zahanati pamoja na stoo, ukarabati wa nyumba za walimu ambazo ni tatu, ukarabati wa matundu 22 ya vyoo na mabafu 24, ununuzi wa meza 100 na viti 100 vya wanafunzi. Na maeneo ambayo yanaendelea kufanyiwa ukarabati ni kufunga madirisha kwenye vyumba vya madarasa 12 na kazi ya kukamilisha viunga.

Hata hivyo amesema kuwa ukamilikaji wa kazi hiyo umechangiwa na umoja wa walimu wa shule hiyo, mhandisi wa Manispaa aliyeshirikiana nao kila siku pamoja na wananchi ambao wameshiriki katika ujenzi kwa namna tofauti wakiwemo mafundi ambao ni wananchi wa eneo hilo.

Kwa upande wake, Mjumbe wa kamati ya Siasa Mkoa ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Ruvuma Oddo Mwisho amesema kuwa wameridhishwa na ukarabati uliofanyika katika shule hiyo ambao ni mfano wa kuigwa katika miradi mingine inayotekelezwa katika Mkoa wa Ruvuma.

“Tunachokiona kinaendana na thamani ya fedha iliyotolewa katika kutekeleza mradi huu.” Amesema Mwisho.

Shule ya Sekondari ya Wavulana Songea ina idadi ya wanafunzi 820 kidato cha kwanza hadi cha sita. Kati ya hao, wanafunzi 40 ni wenye mahitaji maalum ambao wapo kidato cha kwanza mpaka cha nne. Shule hii ni moja ya shule kongwe Tanzania, iliyoanzishwa mwaka 1950 ikiwa na wanafunzi 30.

## II.UKARABATI SEKONDARI KONGWE YA TUNDURU



SERIKALI ya Awamu ya Tano imetoa shilingi milioni 798 kwa ajili ya kukarabati sekondari kongwe ya wavulana Tunduru mkoani Ruvuma yenye wanafunzi zaidi ya 700 ambayo ilianzishwa mwaka 1978.

Mkuu wa shule hiyo Limia Ausi amesema Serikali kupitia Wizara ya Elimu imetoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya kukarabati madarasa,mabweni,ujenzi wa choo kipya,banda la mlinzi na kwamba nyumba za walimu haziusiki katika ukarabati huo.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo,ukarabati umeanza Agosti mwaka huu na kwamba ukarabati unafanyika huku ratiba ya masomo kwa wanafunzi inaendelea kama kawaida hali ambayo imefanya kazi ya ukarabati kufanyika polepole bila kuathiri masomo ya wanafunzi.

“Inatulazimu wanafunzi kuwahamisha katika baadhi ya madarasa na wakati madarasa yao yanaendelea kukarabatiwa,ujenzi hivi sasa umefikia zaidi ya asilimia 90,tunafanya ukarabati kwa njia ya force akaunti’’,alisema Ausi.

Amesema ukarabati upo katika hatua za mwisho na kwamba tayari umefanyika kwenye jengo la utawala,kwenye vyumba vya madarasa 16,mabweni sita ambapo amesema shule hiyo ilijengwa na Umoja wa Mataifa mwaka 1978 kwa ajili ya watoto wa wakimbizi wakati wa harakati za ukombozi katika nchi zilizopo kusini mwa Afrika.

Hata hivyo amesema baada ya harakati za ukombozi kukamilika umoja wa mataifa waliikabidhi shule hiyo serikalini ambapo serikali ilianza kuwachukuwa wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali nchini na kuwapeleka Tunduru kwa ajili ya elimu ya kidato cha kwanza hadi cha nne.

“Wanafunzi wa kwanza walimaliza kidato cha nne mwaka 1982,hivi sasa sekondari ya Tunduru inachukuwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita pekee ambapo tunatoa combination saba zikiwemo PCM,PCB,PGM,CBG,HGL na HKL’’,alisema Ausi. Amesema kutokana na shule hiyo kujengwa kwa ajili ya harakati za ukombozi,ili kuwaenzi mashujaa wa harakati hizo,shule hiyo imetoa majina ya viongozi mbalimbali wa Afrika kwenye mabweni vile MWL.Nyerere,Samaro Machel,Keneth Kaunda,Robeth Mgabe, Netho,Nkurumah na Mandela.

Mkuu huyo wa shule kwa niaba ya walimu ameishukuru serikali kwa kutoa fedha za ukarabati wa shule hiyo ambayo ilikuwa na majengo chakavu ambayo yalikuwa kero kwa wanafunzi na walimu.

Abdalanus Sala mwanafunzi wa kidato cha sita katika sekondari ya Tunduru ameishukuru serikali kwa kumaliza kero ya mazingira magumu ya miundombinu ya madarasa,vyoo na mabweni ambapo amesema wanafunzi hivi sasa wanasoma kwenye mazingira bora ya kufundishia.

Robson Gatson Mwanafunzi Tunduru Sekondari amepongeza mpango wa serikali kukarabati sekondari kongwe nchini ambapo amesema mwanafunzi amejengewa mazingira mazuri ya kusomea mchana na usiku hali ambayo itaongeza ufaulu katika mitihani yake ya mwisho

Akuzungumza baada ya kukagua sekondari ya Tunduru,Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa,Kuhusu ameridhishwa na ukarabati uliofanyika katika sekondari hiyo ametumia fursa hiyo kumpongeza Mkuu wa Shule, Mwalimu Amini Limia pamoja na kamati ya ujenzi kwa kazi nzuri ya usimamizi waliyoifanya.

Waziri Mkuu amesema Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani ilianzisha mkakati wa kukarabati shule zote kongwe nchini ikiwemo ya Shule ya Sekondari ya Tunduru ambayo ukarabati wake umegharimu zaidi shilingi milioni 700. Mkoa wa Ruvuma umepewa jumla shilingi bilioni 3.7 kwa ajili ya ukarabati wa shule kongwe za sekondari ikiwemo ya Tunduru.

Awali, Mkuu wa Shule hiyo, alisema walipokea zaidi ya shilingi milioni 798 kutoka Serikali kupitia mpango wa EP4R kwa ajili ya ukarabati wa majengo 15 ambayo yalikuwa yanakabiliwa na uchakavu mkubwa kutokana na kujengwa miaka 38 iliyopita.

Alisema ukarabati huo pia ulihusisha ujenzi wa majengo mengine mawili ambayo ni matundu 12 ya vyoo kipya cha wanafunzi na kibanda cha mlinzi. “Majengo yaliyokarabatiwa ni jengo la utawala, bwalo na jiko, madarasa vyumba 16, mabweni sita, jingo la zahanati, jingo la duka na stoo, vyoo majengo manne pamoja na kukarabati mfumo wa maji taka nje ya majengo.”

Shule ya Sekondari Tunduru ni miongoni mwa shule kongwe nchini ambayo ilianzishwa mwaka 1982 na ni ya wavulana kwa kidato cha tano na sita katika michepuo ya PCM, PCB, PGM, CBG, HGL, HGK NA HKL na ina jumla ya wanafunzi 682 na walimu 28.



Moja ya majengo katika sekondari ya Tunduru ambayo yamekarabatiwa na serikali ambapo hapa Waziri Mkuu wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa akikagua shule hiyo

## III.UKARABATI WA SEKONDARI KONGWE YA SONGEA GIRLS



WAKALA wa Majengo Tanzania(TBA) wamekabidhi bweni mjoa katika shule ya sekondari ya wasichana Songea ambalo limekarabatiwa kwa zaidi ya shilingi milioni 102.

Kabla ya kukabidhi bweni hilo umefanyika ukaguzi wa bweni hilo la ghorofa likiwa uwezo wa kuchukua wanafunzi 110.

Ukaguzi umewashirikisha watalaam toka Manispaa ya Songea wakiwemo Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Frowin Komba,Mhandisi wa Ujenzi Karoline Kandonga,Mkuu wa shule ya sekondari ya wasichana Songea Tupoke Ngwala,Mwakilishi wa TBA Mhandisi Eugenics Thomas na viongozi wa serikali ya wanafunzi

Akizungumza baada ya kukabidhi mradi huo Mwakilishi wa TBA Mhandisi Eugenics Thomas amesema ukarabati wa bweni hilo

ulianza Januari 10 mwaka huu na kwamba ukarabati wa mabweni mengine matano unaendelea kufanywa katika shule hiyo kwa awamu na kwamba ukarabati wa bweni la pili unaanza rasmi Aprili mwaka huu.

Ametoa rai kwa wanafunzi wa shule ya sekondari ya wasichana ambao wataingia katika bweni hilo lenye vitanda 110 na makabati 110 kuhakikisha wanatunza bweni hilo kwa kuwa serikali imetumia fedha nyingi za kukarabati.

Kwa upande wake Mkuu wa shule ya sekondari ya wasichana Songea Tupoke Ngwala amesema serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 1.6 kwa ajili ya kufanyia ukarabati majengo yote ya shule hiyo yakiwemo mabweni na majengo ya utawala.

Shule ya sekondari ya wasichana Songea ni miongoni mwa shule kongwe nchini ina wanafunzi 874 wanaosoma kidato cha tano na sita ambayo ilianzishwa mwaka 1974.



Baadhi ya majengo katika sekondari ya Songea Girls ambayo yamekarabatiwa na serikali

## IV.UKARABATI SEKONDARI KONGWE YA KIGONSERA




SHULE ya sekondari ya Kigonsera iliyopo wilayani Mbinga mkoani Ruvuma ina historia ya kipekee hapa nchini kwa sababu ndiyo sekondari iliyoweza kuwatoa viongozi wawili wa ngazi ya juu kabisa nchini.

Ponsiano Ngungulu ni Mkuu wa sekondari ya Kigonsera anasema shule hiyo ilianzishwa mwaka 1938 ikiwa ni seminari ya kanisa katoliki chini ya Shrika la Wabenedikitini(Benedictine fathers) wa Peramiho hadi mwaka 1961 ilipochukuliwa na serikali.

Ngungulu anasema shule hiyo ya wavulana pekee, ina uwezo wa kuwahudumia wanafunzi 280 na kwamba tangu kuanzishwa kwake hadi sasa,shule hiyo imeweza kutoa jumla ya wahitimu 13,266.

“Shule wakati inaanzishwa na wakoloni ilikuwa na lengo la kutoa elimu ya dini ya kikristo hususani dhehebu la kanisa katoliki hivyo baada ya uhuru serikali iliamua kuitaifish ili iweze kuwahudumia watanzania wote bila ubaguzi wa kidini’’,anasema.

Hata hivyo anasema tangu mwaka 1961 hadi mwaka 2011 sekondari ya Kigonsera imekuwa inatoa elimu ya sekondari kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne na kuanzia mwaka 1998 hadi sasa sekondari hiyo imekuwa inatoa elimu ya kidato cha sita.

Sekondari ya Kigonsera imepata umaarufu mkubwa hapa nchini kwa sababu imeweka historia iliyotukuka baada ya viongozi maarufu wa kitaifa kusoma katika sekondari hiyo.

Mkuu wa sekondari ya Kigonsera anamtaja mmoja wa viongozi hao kuwa ni Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Benjamin Mkapa ambaye alisoma Kigonsera toka mwaka 1952 hadi 1953 kisha alihamia Ndanda mkoani Mtwara.

Ngungulu anamtaja Kiongozi mwingine wa kitaifa ambaye amesoma Kigonsera ni Waziri Mkuu wa Tanzania Kassim Majaliwa ambaye alianza kidato cha kwanza na kuhitimu kidato cha nne katika sekondari hiyo mwaka 1980.

Licha ya viongozi hao sekondari ya Kigonsera imetoa viongozi wengine wengi hapa nchini ,miongoni mwao ni Dkt Modestus Kipilimba ambaye ni Balozi wa Tanzania nchini Msumbiji,Profesa Simon Mbilinyi aliyewahi kuwa Waziri wa Fedha na Mbunge wa Peramiho na Juma Homera Mkuu wa Mkoa wa Katavi.

Viongozi wengine waliosoma Kigonsera ni Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Dkt Frolens Turuka,Hayati Askofu Mstaafu wa Jimbo la Mbinga Imanuel Mapunda,Hayati Askofu Mstaafu wa Jimbo la Njombe Raymund Mwanyika ,Askofu Mkuu Mstaafu wa Jimbo Kuu la Songea Norbeth Mtega,Askofu wa Jimbo la Lindi Mhashamu Bruno Ngonyani ,Askofu wa Jimbo la Mtwara Mhashamu Gabriel Mmole na Askofu wa Jimbo la Njombe Mhashamu Alfred Maluma .

Mkuu wa shule anawataja walimu waliopo hivi sasa katika sekondari hiyo kuwa ni 37 na kwamba idadi ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita kwa mwaka 2019/2020 wanafikia 776 kati yao 414 ni wa kidato cha tano na 362 ni wa kidato cha sita.

Shule ya sekondari ya kigonsera kwa miaka mitatu mfululizo imekuwa inafanya vizuri kitaaluma ,mwaka 2017 tulifaulisha kwa asilima 97,mwaka mwaka 2018 kwa asilimia 98 na mwaka 2019,tulifaulisha kwa asilimia 99.52’’,anasema Ngungulu.

Licha ya mafanikio yaliyopatikana Mkuu wa shule hiyo anazitaja changamoto zinazoikabili shule hiyo kuwa ni ubovu wa barabara ya kuingilia shuleni,uchakavu wa nyumba 18 za walimu na ukosefu wa watumishi wasiokuwa walimu hasa wapishi,dereva,karani na wahudumu wa ofisi ya Mganga.

Changamoto nyingine anazitaja kuwa ni upungufu wa walimu sita wa masomo ya Sayansi,uchakavu wa magari ya shule,ukosefu wa maktaba,zana hafifu za kilimo ili kuwafundisha wanafunzi kilimo cha kisasa kinachoendana na sera ya viwanda na upungufu wa fedha za kununulia vifaa vya Sayansi na kemikali.

Hata hivyo anasema katika kujiongezea mapato shule hiyo inafanya elimu ya kujitegemea ambapo shule inamiliki shamba la

ekari 30 na katika msimu wa kilimo wa mwaka 2018/2019 wamefanikiwa kuvuna jumla ya tani 26 za mahindi na kwa kwamba shule pia ina mradi wa ng'ombe saba.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas akizungumza baada ya kutembelea shule hiyo, anaishukuru serikali kwa kutoa zaidi ya milioni 930 za kukarabati sekondari hiyo kongwe nchini ambayo majengo yake yalikuwa yamechakaa.

Amesema mazingira ya shule hiyo yamekuwa rafiki baada ya ukarabati mkubwa wa majengo mbalimbali ya shule na nyumba mbili za walimu ambapo hivi sasa muonekano wa shule hiyo unavutia.

Hata hivyo amewaagiza TARURA wilaya ya Mbinga kukarabati barabara inayofika katika shule hiyo ili iweze kupitika wakati wote ikiwa ni sehemu ya kuwaenzi viongozi wa kitaifa ambao wamesoma katika shule hiyo .

“Lazima tuendelee kuitunza historia ya shule hii kwa kusomesha viongozi wa kitaifa Rais Mstaafu Mkapa na Waziri Mkuu Majaliwa wamesoma hapa,ni lazima changamoto zote zinazoikabili shule zitafutiwe ufumbuzi,shule hii ni urtihi wetu katika Mkoa wa Ruvuma’’,anasisitiza.

Moto wa shule ya sekondari ya Kigonsera, Elimu ni ukombozi na dira ya shule ni kutoa elimu bora ya kupambana na changamoto mbalimbali zinazotokana na mabadiliko ya Dunia.

## SURA YA SABA

## UJENZI WA VYUO VYA VETA MKOANI RUVUMA

Eneo hili linajumuisha utoaji wa elimu katika vyuo vya ufundi (VETA) na vyuo vya ufundi stadi vya kati. Kwa sasa Mkoa una vyuo 3 ambavyo vinatoa huduma ya ufundi ambavyo ni VETA Songea,Namtumbo na Nyasa.



Mkuu wa chuo cha VETA Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma Mhandisi Lulu Chilumba akizungumzia kozi cha chuo hicho



## A.CHUO CHA UFUNDI STADI WILAYA YA NYASA



UJENZI wa chuo cha ufundi Stadi VETA Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma uliogharimu zaidi ya shilingi bilioni mbili umekamilika.

Mkuu wa chuo hicho Mhandisi Lulu Chilumba amesema chuo kinatarajia kuanza mafunzo mwaka 2023.

Amesema chuo linatarajia kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ili kuhakikisha vijana wanapata mafunzo yatakayowawezesha kuajiriwa au kujiajiri.

“Kwa kuanzia tunaanza na kozi sita katika fani za uhazili,ujenzi,umeme,Seremala,ubunifu wa mavazi,ushonaji na ufundi wa magari “,alisema Mhandisi Chilumba.

Hata hivyo amesema fomu za kujiunga na chuo hicho zinatolewa chuoni Nyasa au kwenye tovuti ya VETA ambapo maombi ya kujiunga yalianza Septemba hadi Oktoba 2022.

Mbunge wa Jimbo la Nyasa Mhandisi Stella Manyanya ametoa rai kwa wananchi wa jimbo lake kukitumia chuo cha VETA Nyasa ambacho serikali imewasogezea hadi mlangoni

Mhandisi Manyanya amesema kwa miaka mingi wananchi walikuwa wanapata shida ya kusafiri mbali kufuata chuo cha VETA Songea au Namtumbo.

“Kwa niaba ya wananchi wa Nyasa tunaishukuru serikali kwa kusimamia na kutekeleza kwa vitendo Ilani ya CCM kupitia mradi huu ambao utawanufaisha vijana wa Nyasa’’,alisisitiza Mhandisi Manyanya.

Kukamilika kwa chuo hiki kunaufanya Mkoa wa Ruvuma kuwa na vyuo vitatu vya VETA ambavyo ni Nyasa,Songea na Namtumbo, katika nchi nzima kuna vyuo vya VETA 46.



Moja ya majengo katika chuo cha VETA wilayani Nyasa mkoani Ruvuma

## C.CHUO CHA VETA SONGEA KILIVYOPUNGUZA TATIZO LA AJIRA KWA VIJANA



Mafunzo ya Ufundi Stadi VETA Songea yalianza kutolewa mwaka 1984 kwa kutumia majengo yaliokuwepo katika viwanja vya Sabasaba vilivyopo Matarawe Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Katika kipindi hicho chuo kilikuwa na uwezo wa kutoa mafunzo kwa wanafunzi 60 tu katika fani tatu ambazo ni ufundi magari,ujenzi na useremala.

Mkuu wa Chuo cha Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi VETA Songea Gideon Ole Lairumbe anasema ujenzi wa majengo ya kudumu ya chuo hicho katika eneo la Msamala Manispaa ya Songea ulianza mwaka 2003 na kukamilika mwaka 2005.

Lairumbe anabainisha kuwa ujenzi huo ulijumuisha karakana tisa za mafunzo,jengo la utawala, maktaba, madarasa,jengo la maliwato,uzio na chumba cha mitambo ya umeme.

Anabainisha kuwa katika ujenzi huo zaidi ya sh.bilioni 1.654 zilitumika kati ya fedha hizo ujenzi wa majengo zilitumika zaidi ya sh.milioni 975,Mshauri elekezi zaidi ya sh.milioni 86.45 na ununuzi wa mitambo na vifaa vya mafunzo zilitumika zaidi ya sh.milioni 592.

Anasema baada ya ujenzi wa chuo hicho kukamilika ,uwezo wa kudahili wanafunzi katika chuo umeongezeka toka wanafunzi 60 hadi 250 kwa mwaka.

Hata hivyo Mkuu huyo wa chuo anabainisha kuwa  hadi kufikia mwaka 2017 chuo hicho kina wanachuo 646 kati yao wanachuo wanaosomea hatua ya kwanza(level one) wanaume 253 na wanawake 88,wanaosomea hatua ya pili wanaume ni 176 na wanawake 67 na wanaosomea hatua ya tatu wanaume ni 55 na wanawake saba.

"Chuo kinatoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi,kwa kozi za muda mrefu mafunzo yanayotolewa ni katika fani za ufundi magari,uungaji vyuma,umeme wa magari,umeme wa majumba, useremala,uashi,ufundi bomba,ushonaji na uhazili na kompyta'', anasema Lairumbe.

Kwa mujibu wa Mkuu huyo hadi sasa wanafunzi ambao wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu ni 591 na kwamba chuo hicho bado kinaendelea kupokea wanafunzi wa mwaka wa kwanza na kwamba mafunzo yanatolewa katika awamu mbili tofauti asubuhi na mchana.

Mkuu huyo wa Chuo anayataja mafunzo ya muda mfupi  yanayotolewa na VETA Songea kuwa ni fani za udereva wa magari daraja D,udereva wa magari ya abiria na uhazili.

Fani nyingine ni ukarabati wa kompyuta,utumiaji wa kompyuta,umeme wa majumba,umeme wa jua, ulimbwende(cosmetology),utengenezaji wa dawa za usafi, sabuni za maji,upishi na utengenezaji wa batiki na ujasirimali.

Takwimu zinaonesha kuwa tangu kuanzishwa kwa chuo hicho hadi kufikia mwaka 2016 wahitimu wa mafunzo ya muda mfupi ni 3013 kati yao wasichana 523 na wavulana 2490.

Miongoni mwa walionufaika na VETA Songea ni wahitimu wa kwanza 20 wa fani ya ushonaji ambao walikabidhiwa vifaa vya ushonaji  vyenye thamani ya sh.milioni 10  kwa ajili ya kuwajengea uwezo wahitimu wa fani ya ushonaji kabla ya  hawajaingia rasmi kwenye soko la ajira.

“Chuo kiliamua kuanza na fani ya ushonaji kuwapa motisha ya vifaa kutokana na uzoefu kuonesha kuwa wanaojiunga na fani hii wengi ni wanafunzi wa kike ambao pi waathirika zaidi wa ukosefu wa ajira ni nchini’’,anasema Mkuu wa Chuo.

Anasema kuwa chuo hicho kimefanikiwa kupata jengo jipya ambalo linajumuisha maabara za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano(TEHAMA),madarasa na ofisi za walimu.

Sanjari na ufundishaji wa kozi fupi,Mkuu huyo wa chuo anasema chuo kimekuwa kinafundisha kozi fupi za udereva wa pikipiki,udereva wa magari,utengenezaji wa sabuni na batiki na kwamba lengo ni kuwafikia wahitaji wote mahali walipo ili kupunguza changamoto ya ajira.

Licha ya kutoa kozi hizo katika Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma,Mkuu wa Chuo hicho anasema,VETA Songea pia imefanikiwa kufundisha kozi hizo katika wilaya za Njombe,Ludewa na Makete mkoani Njombe.

“Chuo pia kinatoa mafunzo kwa kushirikiana na viwanda na maeneo mbalimbali ya kazi,lengo likiwa ni kuwajengea uwezo zaidi wafanyakazi viwandani ili kuongeza tija’’,anasema Lairumbe.

Anasema VETA Songea inashirikiana na viwanda na kampuni mbalimbali zikiwemo UNILEVER ambayo ni kampuni ya kiwanda cha chai,Kampuni ya MANTRA ya mgodi wa uranium na kampuni ya Food Security ambayo wafanyakazi wake 31 wamepata mafunzo ya muda mfupi kupitia VETA.

Anayataja matarajio ya chuo hicho kuwa ni kuanzisha fani ya uandaaji wa vyakula(Food Production),utengenezaji wa vifaa vya kilimo(Agro Mechanics) na kozi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano(TEHAMA).

Anatoa rai kwa serikali na wadau wengine kuiangalia VETA kama mkombozi wa ajira kwa vijana hasa katika kipindi hiki ambacho Tanzania na Dunia nzima inakabiliwa na janga la ukosefu wa ajira ambapo vijana ndiyo waathirika wakuu.

Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda wakati anafungua chuo cha VETA Songea mwaka 2013,pamoja na mambo mengine aliagiza Wizara ya Elimu

na Mafunzo ya Ufundi kusaidia kuongeza nafasi za mafunzo katika vyuo vya VETA ili vijana wengi wanaomaliza shule za msingi na sekondari waweze kupata nafasi ya kujifunza kozi mbalimbali ambazo zitawawezesha kuajiriwa na kujiajiri.



Baadhi ya wanachuo wa VETA Songea wakiwa kwenye mazoezi ya vitendo katika fani za ushonaji na ufundi kujenga



## D.CHUO CHA UFUNDI STADI VETA WILAYANI NAMTUMBO



Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma ambacho kilizinduliwa na Rais wa Awamu ya Tano Dkt.John Magufuli kilichojengwa na Serikali ya Tanzania kwa gharama ya shilingi Bilioni 6.5 na ambacho kitakuwa na uwezo wa kutoa mafunzo kwa wanafunzi 600 wa kozi ndefu na fupi kwa mwaka. Mradi huu unajumuisha ujenzi wa majengo 14 pamoja na kazi ya kutengeneza mazingira ya nje.

Majengo yanayojengwa ni jengo lautawala,madarasa manne,vyoo,jengo la karakana ya ufundi bomba na ushonaji,majengo mengine ni karakana yauseremala, uashi,umakenika wa mitambo mizito,karakana ya umeme wa majumbani,jengo la maktaba,jengo la stoo na kibanda cha jenereta,



## SURA YA NANE:

## ELIMU NYINGINE ZINAZOTOLEWA MKOANI RUVUMA

### 1.Elimu Maalum, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi



***Jengo la Mamlaka ya Elimu Tanzania TEA ambalo limejengwa Lituhi wilayani Nyasa mkoani Ruvuma***

Utoaji wa elimu unahusisha Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ambayo ni Elimu Endelevu inayotekelezwa katika Halmashauri zote nane za Mkoa wa Ruvuma. Elimu Nje ya Mfumo Rasmi inayojumuisha Elimu ya Msingi kwa watoto walioikosa (MEMKWA), Mpango wa Elimu ya Sekondari kupitia Ujifunzaji huria (Open Learning) unaojumuisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wa mtihani wa Maarifa (QT). Elimu ya Watu Wazima inahusisha utoaji wa stadi za Kisomo (KKK) kwa watu wazima na Kisomo cha kujiendeleza kwa kupiga vita Umasikini, Maradhi na Ujinga ili kumudu

mazingira na kujiletea maendeleo kupitia Elimu ya Ufundi Stadi na shughuli za kijamii na za uzalishaji mali (shughuli za kiuchumi).

Hadi kufikia Novemba, 2022 kuna vituo **109** katika shule za msingi vinavyotekeleza Mpango wa Elimu ya Msingi kwa watoto walioikosa (MEMKWA). Utekelezaji wa Mpango wa Elimu ya sekondari katika vituo **125** vinavyoaandaa wanafunzi wa mtihani wa Maarifa **(QT)** na utekelezaji wa elimu ya ufundi stadi katika vituo vya ufundi stadi **24**.

Utekelezaji wa **elimu maalum** unafanyika katika shule zote za msingi na sekondari. Kwa sasa kuna vituo **302** katika shule zilizobainisha watoto wenye mahitaji maalum. Ubainishaji kwa ajili ya usajili wa wanafunzi wenye mahitaji maalum hufanyika kila mwaka kwa ajili ya uandikishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa mwaka wa masomo unaofuata.



Pichani ni shule maalum ya Viziwi ya St,Vinsent iliyopo Ruhuwiko Manispaa ya Songea inayotoa elimu ya msingi

## 2.WATOTO WENYE 149 ULEMAVU WAGUNDULIKA MADABA



Afisa Elimu Maalum katika Halmashauri ya Madaba wilayani Songea mkoani Ruvuma Teddy Sanga amesema hadi sasa katika Halmashauri hiyo wamebainika jumla ya watoto wenye ulemavu 149 ambao wanasoma katika shule za msingi zilizopo katika Halmashauri hiyo..

Amesema kati ya watoto hao wavulana ni 80 na wasichana ni 69 na kwamba katika mwaka wa masomo 2022/2023 wanafunzi 29 wenye ulemavu wameandikishwa na kuanza masomo masomo,hivyo ametoa rai kwa wazazi na walezi kutowafungua ndani watoto wenye ulemavu kwa sababu wana haki ya kupata elimu kama walivyo watoto wasiokuwa na ulemavu.



## 3.HALMASHAURI YA SONGEA YAJENGA SHULE MPYA YA ELIMU MAALUM



HALMASHAURI ya wilaya ya Songea mkoani Ruvuma,imepokea kiasi cha Sh.milioni 380 kutoka Serikali kuu kwa ajili ya kujenga vyumba 19 vya madarasa kwenye shule shikizi zilizojengwa kwenye maeneo yenye mazingira magumu ya kupata elimu kwa wanafunzi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo Neema Maghembe alisema,fedha hizo zimetumika kujenga jumla ya shule mpya tano za msingi ikiwamo shule ya Lihuhu ili kuwanusuru watoto wenye umri wa kuanza shule kukosa haki ya kupata elimu.

Maghembe alisema,awali wanafunzi wanaotoka katika kijiji cha Lihuhu walilazimika kutembea umbali wa km 7 kwenda kijiji cha Lilahi kufuata shule, hivyo kusababisha baadhi yao kukatisha masomo.

Alisema,katika kijiji hicho ambacho mwanzo kilikuwa kama kitongoji cha kijiji mama cha Lilahi,serikali imejenga jumla ya madarasa matatu kwa gharama ya Sh.milioni 60 ikiwa ni mkakati wake wa kuimarisha na kuboresha miundombinu ya elimu.

Alisema,baada ya kukamilika kwa ujenzi wa vyumba hivyo,sasa wanafunzi wamekuwa na mazingira mazuri ya kujisomea na walimu kuwa na muda mzuri ya kufundisha ikilinganishwa na awali ambapo kulikuwa na madarasa ya miti yaliyojengwa na wananchi.

Maghembe alitaja shule zilizojengwa kupitia fedha hizo ni Jenista Mhagama, ambapo serikali imejenga vyumba vitatu kwa gharama ya Sh.milioni 60 na shule ya msingi Lunyele madarasa matatu kwa Sh.milioni 60.

Shule nyingine zilizonufaika na fedha hizo ni Mhimbasi iliyopata madarasa matano kwa gharama ya Sh.milioni 100 na kata ya Kizuka ambapo imejengwa shule mpya yenye madarasa Matano kwa gharama ya Sh.milioni 100.

Alisema,serikali inaendelea kufanya juhudi kubwa kuhakikisha kila mtoto mwenye umri wa kuanza elimu ya awali,msingi na sekondari anapata elimu na kuwaomba wazazi,walezi na jamii kwa ujumla kushiriki na kujitolea nguvu zao kujenga na kuboresha miundombinu ya elimu.

Baadhi ya walimu wa shule hizo, wameipongeza Serikali kwa jitihada zake za kujenga na kuboresha miundombinu ya elimu katika maeneo mbalimbali.

Mwalimu mkuu wa shule ya Lihuhu Simon Pascal alisema kuwa, madarasa hayo mapya yamehamasisha sana wanafunzi kuhudhuria masomo na kukomesha tatizo la utoro na kurudisha morali ya kufundisha kwa walimu.

Mwalimu Pascal alisema,baada ya kujengwa madarasa mpya hata idadi ya watoto wanaoanza darasa la kwanza imeongezeka kutoka 20 mwaka wa masomo 2020/2021 hadi 45 kwa mwaka wa masomo 2021/2022.

Mwalimu wa shule ya msingi Lunyele kata ya Muhukuru Silvesta Ngumba,ameiomba serikali kupitia Halmashauri ya wilaya kuwasaidia

walimu wanaofanya kazi kwenye maeneo yenye mazingira magumu kwa kutoa motisha na kuboresha mazingira yao.

Alisema,licha ya serikali kujenga vyumba vipya vya madarasa kwa ajili ya kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia,hata hivyo kwa upande wa walimu bado wanakabiliwa na mazingira magumu. Alisema,changamoto kubwa hasa ni makazi kwani katika shule hiyo kuna walimu watano ambao wanaishi kwenye nyumba moja ambayo haina hadhi ya kuishi mtumishi wa umma.

Aidha alisema, hata wanapohitaji kufika makao makuu ya Halmashauri ya wilaya au Songea mjini, wanalazimika kutumia zaidi ya shilingi 50,000 kama nauli,hivyo ameiomba serikali kuwaangalia kwa jicho la huruma watumishi waliokubali kufanya kazi kwenye mazingira hayo.



## 4.MKUU WA MKOA WA RUVUMA AZINDUA MIONGOZO MITATU YA ELIMU



MKUU wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas amezindua miongozo mitatu ya usimamizi na uendeshaji wa elimu.

Hafla ya uzinduzi huo imehudhuriwa na wadau wa elimu kutoka wilaya zote tano za Mkoa wa Ruvuma na kufanyika katika ukumbi wa shule ya sekondari ya Songea Girls mjini Songea.

Akizungumza kabla ya kuzindua miongozo hiyo Kanali Thomas amewaagiza wasimamizi wa elimu kusimamia na kuondoa changamoto ya baadhi ya wanafunzi kutomudu stadi za Kuandika,Kuhesabu na Kusoma (KKK).

“Mkaondoe udhaifu wa baadhi ya viongozi katika usimamizi na ufuatiliaji,kasimamieni na kuweka mikakati ya kupunguza au kuondoa kabisa uhaba wa miundombinu ya shule hasa vyoo vya wanafunzi’’,alisema RC Thomas.

Mkuu wa Mkoa amewaagiza wadau wote wa elimu kuondoa utoro wa baadhi ya wanafunzi na walimu.
Hata hivyo amesema miongozo hiyo imechambua changamoto mahususi katika elimu ya awali,msingi na sekondari na kwamba mikakati ya muda mfupi na mrefu ya utatuzi wa changamoto imebainishwa katika miongozo hiyo.

Awali Mwakilishi wa Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Jeremiah Sendoro aliitaja miongozo mitatu ambayo imezinduliwa kuwa ni Mwongozo ambao umeainisha changamoto katika elimu ya msingi na sekondari.

Ameutaja mwongozo wa pili kuwa unahusu mkakati wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi ya elimu ya msingi na mwongozo wa tatu umeeleza kuhusu uteuzi wa viongozi wa elimu katika mamlaka za serikali za mitaa na mikoa.

Hata hivyo amesema miongozo yote mitatu imebeba changamoto na taratibu za usimamizi na uendeshaji wa elimu ya msingi na sekondari na kwamba miongozo hiyo inakusudia kuleta tija katika sekta ya elimu kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Naye Afisa Elimu Mkoa wa Ruvuma Emanuel Kisongo amesema miongozo hiyo inatarajia kuwa ni muarubaini wa changamoto za elimu hapa nchini.
Kisongo amesisitiza kuwa miongozo hiyo imebeba zana ya kurudi darasani na kuwapa wanafunzi kile kinachostahili na kwamba wadau wote wa elimu wanatakiwa kusimamia kikamilifu utoaji elimu.

Miongozo hiyo mitatu imeundwa Julai mwaka huu kupitia Wizara ya TAMISEMI ikiwa ni juhudi za serikali ya awamu ya sita kuboresha elimu ili wananchi wake wapate elimu bora na kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya Tanzania.



# SURA YA TISA

## HABARI PICHA SEKTA YA ELIMU MKOANI RUVUMA.

## 1,UKAGUZI MRADI WA SEKONDARI YA LIMBU WILAYA YA NYASA



Menejimenti ya Mkoa wa Ruvuma ikiongozwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Ndugu Stephen Ndaki imekagua mradi wa ujenzi wa madarasa matatu yaliyogharimu shilingi milioni 60 katika shule ya sekondari ya Limbo wilaya ya Nyasa Akizungumza baada ya kukagua mradi huo Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma ameipongeza Halmashauri ya Nyasa kwa kutekeleza mradi huo ambao umekamilika na wanafunzi wameanza kuyatumia.

Hata hivyo Ndaki ameitaja changamoto kubwa katika utekelezaji wa miradi ni usimamizi hafifu hasa katika umaliziaji kwenye framu na milango

## 2,RAS RUVUMA AKERWA NA MATOKEO MABAYA KIDATO CHA NNE MAKITA SEKONDARI



KATIBU Tawala Mkoa wa Ruvuma Ndugu Stephen Ndaki akiwa na Menejimenti Mkoa amefanya ziara ya kikazi ya kukagua mradi wa ujenzi wa madarasa mawili yaliyogharimu shilingi milioni 40 katika shule ya sekondari Makita iliyopo Halmashauri ya Mji wa Mbinga.

Hata hivyo taarifa ya taaluma ya sekondari hiyo katika matokeo ya kidato cha nne imemsikitisha Katibu Tawala huyo baada ya kuelezwa kuwa wanafunzi 85 kati ya wanafunzi 174 waliofanya mtihani wa kidato cha nne 2022 wamepata daraja la nne na sifuri ni zaidi ya nusu ya darasa

kulingana na Baraza la Mitihani matokeo ya kidato cha nne mwaka 2022 katika sekondari hiyo yanaonesha kuwa daraja la kwanza wapo 11,daraja la pili 33 daraja la nne 80 na sifuli watano

Ndaki amewataka walimu wa shule hiyo ambao ni zaidi ya 47 kufundisha kwa bidii ili wanafunzi wengi waweze kufaulu mtihani wa kidato cha nne ambapo ametahadharisha kuwa katika mtihani wa mwaka huu hataki kusikia hali hiyo inajirudia tena vinginevyo atachukua hatua kali.

## 3.MENEJIMENTI RUVUMA YAPONGEZA UJENZI WA SEKONDARI YA LUSONGA



MENEJIMENTI Mkoa wa Ruvuma ikiongozwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Ndugu Stephen Ndaki imekagua mradi wa ujenzi wa sekondari mpya Kata ya Lusonga Halmashauri ya Mji Mbinga ambayo serikali ya awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan ilitoa shilingi milioni 470 kutekeleza mradi huo ambao tayari shule imesajiriwa na wanafunzi wameanza masomo.

Menejimenti hiyo imesema imetembelea shule mbalimbali katika Mkoa wa Ruvuma zinazotekeleza mradi wa programu ya uboreshaji elimu ya sekondari SEQUIP, ambapo Halmashauri ya mji wa Mbinga imetekeleza mradi huo kwa ufanisi mkubwa ukilinganisha na Halmashauri nyingine hivyo wanastahili pongezi.



## 4.SEKONDARI YA MFANO WILAYANI MBINGA




Sekondari mpya ya Lusonga iliyojengwa katika Halmashauri ya Mji Mbinga,miongoni mwa sekondari mpya 11 ambazo serikali ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan imetoa jumla ya shilingi bilioni 7.7 kujenga sekondari hizo mkoani Ruvuma kupitia program ya Uboreshaji Elimu ya sekondari SEQUIP

## 5.SEKONDARI MPYA HALMASHAURI YA MADABA




Shule mpya ya sekondari ya Joseph Kizito iliyojengwa Kata ya Lituta Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma

Serikali imetoa shilingi bilioni 7.7 kujenga shule mpya 11 za sekondari katika Mkoa wa Ruvuma


## 6.RC RUVUMA AKAGUA UJENZI WA SEKONDARI YA MKOA WA RUVUMA



Kushoto mwenye suti ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas akizungumza wakati anakagua mradi wa ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya Mkoa ya wasichana inayojengwa eneo la Migelegele Wilaya ya Namtumbo kwa gharama ya shilingi bilioni tatu



## 7.MKUU WA MKOA AKAGUA SAMANI ZA SEKONDARI YA MKOA WA RUVUMA



Kushoto mwenye suti ni Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas akikagua ubora wa viti na meza 80 zilizotengenezwa kwa ajili ya shule ya sekondari mpya ya Mkoa ya Wasichana inayoendelea kujengwa katika eneo la Migelegele Wilaya ya Namtumbo kwa gharama ya shilingi bilioni tatu .Sekondari hiyo inayotarajia kuanza kuchukua wanafunzi mwaka 2023 ni miongoni mwa sekondari mpya kumi za mikoa za wasichana zinazojengwa na serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan.



## 8. SEKONDARI YA MFANO MKOANI RUVUMA




SERIKALI kupitia program ya SEQUIP imetumia shilingi milioni 470 kujenga sekondari mpya ya Joseph Kizito kata ya Lituta Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma

## 9.PROGRAMU YA SEQUIP MKOANI RUVUMA




Serikali imetoa shilingi bilioni 7.7 kupitia program ya Uboreshaji Elimu ya Sekondari nchini SEQUIP kujenga shule mpya 11 za sekondari mkoani Ruvuma

## 10.ZIARA YA RC RUVUMA UKAGUZI WA MIRADI YA ELIMU



MKUU wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Laban Thomas wa kwanza kushoto akitoa maelekezo baada ya kukagua miradi ya maendeleo katika Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea

## 11.SEKONDARI YA MFANO MANISPAA YA SONGEA



shule mpya ya sekondari ya Luhira Manispaa ya Songea imekuwa kivutio kutokana na muonekano wake.

Shule hii imejengwa kupitia Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP) .

## 12.MILIONI 470 ZILIVYOTEKELEZA MRADI WA SEKONDARI MPYA HALMASHAURI YA SONGEA




Menejimenti ya Mkoa wa Ruvuma ikiongozwa na Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Ndugu Stephen Ndaki imefanya ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya ya Songea.

Moja ya miradi iliyokaguliwa ni ujenzi wa sekondari mpya ya Kizuka katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea ambapo hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 85.

Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 470 kujenga Majengo ya Utawala,madarasa manane maabara tatu,jengo la maktaba na TEHAMA.

**JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**OFISI YA MKUU WA MKOA WA RUVUMA**

**1 BARABARA YA TUNDURU**

**S.L.P 74 SONGEA**

**57180 RUVUMA**
**SIMU Nambari.025- 2602256/2602238**
**FAX Na.2602144**
**E-MAIL:** ras.ruvuma@tamisemi.go.tz
**TOVUTI:www.ruvuma.go.tz**
**INSTAGRAM; kusini_News**

**FACEBOOK: kusini_News**

**TWITTER:kusini_News**

**YOU TUBE;kusini News**